# Chujio la Mtu Mwenye Busara

Jeffersonville, Indiana USA

Agosti 22, 1965

1 Asante, Ndugu Mann. Niliona ulimleta ndugu. Bwana awabariki. "Mambo yote yanawezekana, amini tu." Hebu na tuombe.

Ee Mungu, kweli hivyo ndivyo shauku ya moyo wetu ilivyo usiku wa leo, kuamini tu. Kama tulivyokusanyika hapa usiku wa leo katika maskani, jua likitua magharibi, tunaomba, Mungu mpendwa, ya kwamba utatujalia kutambua jinsi lilivyo karibu kwamba jua linatua pia kwa wakati; unakwisha. Siku imekwisha. Nasi tunakumbuka wakati mmoja wakati siku ilikuwa imekwisha, wasafiri wawili walikuomba uingie ukae pamoja nao. Na ndipo ukajitambulisha kwao kwa kueleza Neno Lako na kuwafanya waone yale ambayo Kristo hana budi kuteseka, mambo haya yote kwanza.

Kwa hiyo tunaomba, Mungu, kwa kuwa siku imekwisha, kwamba utaingia katika nyumba zetu na kuishi pamoja nasi, na utuelezee Neno, Bwana, ambalo kwa neema tunalishikilia kama hazina kutoka Kwako, kama karama katika mioyo yetu. Jalia kamwe tusiivuke; jalia sikuzote tuiheshimu kwa mioyo yetu yote.

Tunakushukuru kwa ajili ya yale uliyowafanyia wale walio hospitalini asubuhi ya leo, na yale uliyomfanyia mvulana mdogo wa Ndugu Capps aliyekuwa amelala, karibu afe, na sasa huyu hapa katika wasikilizaji usiku wa leo. Jinsi tunavyokushukuru Wewe, Baba, kwa ajili ya mambo haya yote!

Tujalie, Bwana, tupate kujua jinsi ambavyo tunapaswa kukupa sifa. Tunaninii tu … Ni zaidi ya ufahamu wetu kujua jinsi ya kukupa sifa. Lakini, Bwana, pokea mioyo yetu kama ishara za shukrani, ya kwamba tunakupenda. Na wakati tu—tunapotaka kufanya yaliyo mema, tuonyeshe la kufanya. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mnaweza kuketi.

2 Habari za jioni kwa kanisa hili kubwa lililojaa watu usiku wa leo na kote nchini kwa simu. Wanasema wameunganishwa tena usiku wa leo.

Natumaini mke wangu anasikiliza. Sikuweza kumpigia simu, kwa hiyo nitampigia simu baada ya ibada hii.

Nasi tuna maandishi hapa ya kwamba asubuhi ya leo ndugu wa Ndugu Jackson … ama baba akiwa katika hali kama hiyo, kwamba hali yake imeimarika, huenda akaja nyumbani kesho.

Mvulana mdogo wa Ndugu Capps, ambaye aliniita hivi majuzi usiku, sijui kama Ndugu Capps katika wasikilizaji ama la, lakini, na mvulana wake mdogo alikuwa mgonjwa sana.

Na ilitukia tu kwamba mimi na Joseph tulikuwa tuko kule kwenye—kwenye safu ya kupigia shabaha, nikiandaa bunduki yangu ndogo ya ishirini na mbili. Niliwaambia yote kuhusu hilo juma lililopita. Naye kweli atakuwa mlenga shabaha kweli. Na kwa hiyo alitaka kuwa na hakika na kumwambia Gary na Larry yale aliyofanya. Naye akaniambia, tukirudi … Nikasema, "Unapaswa kusimama na—na kumwambia Ndugu Gene Norman kuhusu hilo."

Akasema, "Simama na umwambie Billy kwanza," ndugu yake.

Baada ya kumwonyesha shabaha nzuri alizopiga, akasema, "Sasa kaa mbali ya miguu yangu." Mnaona?

3 Na tulipofika tu pale, mbona, simu ikalia, na Billy akaingia ndani mbio kuuliza … Nikasema, "Huenda ikawa ni simu toka kwa mgonjwa sasa." Nasi tukaingia tu ndani, na ilikuwa Ndugu Capps. Naye mvulana huyo mdogo alikuwa na ugonjwa wa uvimbe wa tumbo, na alikuwa na nafasi ndogo sana ya kuishi. Na Bwana amemponya. Na usiku wa hivi majuzi alisema anaugua maumivu ya namna fulani, Bibi Woods alikuwa akiniambia. Nasi tulikuwa tukiondoka kwa haraka, nami … Nikasema, "Bibi. Woods, tumechelewa sana sasa, saa nne kamili, nina shaka wao wananiruhusu niingie ndani kule hospitalini." Nikasema, "Ninaenda nyumbani na kufunga tu mlango." Ndipo nikapanda na kuomba. Nao wanasema mvulana huyo mdogo yuko kwenye kusanyiko usiku wa leo. Kwa hiyo tunashukurani sana kwa ajili ya jambo hilo. Nasi tunashukuru.

Sasa tunashikilia; hatujasikia bado. Kama Ndugu Leo Mercier na Dada Mercier wanasikiliza, bado hatujasikia kutoka kwa baba yako. Tunatumaini kusikia katika muda mfupi, jinsi anavyoendelea. Lakini karibu nina hakika atapona, kwa hiyo tunatumaini hilo kwa Mwenyezi Mungu, ya kwamba Mungu atamtunza mtu huyo mpendwa, mzee mtakatifu, mhudumu mkongwe wa Injili.

4 Sasa, loo, kuna mambo mengi sana yanayopaswa kufanywa, na kuna muda mfupi sana kuyafanya, kwa hiyo weka tu juhudi zetu zote sasa katika yale tunayoweza kumfanyia Bwana wetu.

Nilishuka nikaja mapema kidogo. Nami si—sikuwa najisikia vizuri sana. Nilichoka, nilichoka sana, nami

nililala alasiri ya leo. Kamwe … Hata sijala chakula cha jioni bado. Kwa hiyo ni—nikaingia, nikalala tu alasiri yote. Nilijisikia vibaya, hivyo nimelala pale. Na ndipo nikaanza kuomba, nami nikajisikia vizuri zaidi. Ndipo nikaamka, nikavaa nguo zangu, na kuja kanisani.

Kwa hiyo sisi—sisi tunamtumainia Bwana Yesu sasa ya kwamba atabariki juhudi zetu pamoja usiku wa leo, kwa kuwa kote nchini tunajaribu kujiunga na sehemu hii ya Mwili wa Kristo, ambao nimepewa haki ya kuwalisha kondoo Wake. Nami ningejitahidi tu vizuri kadiri nijuavyo, katika kutoa Chakula kizuri ninachojua kwa ajili ya kondoo.

Nami ninangojea kwa hamu ile saa ambapo sisi sote tunaweza kukusanyika mahali pamoja na kuhubiri juu ya hayo Mapigo Saba, na vile Vitasa Saba, na Baragumu, na kadhalika. Yote yanatukia moja kwa moja katika mkusanyiko mmoja. Hiyo ndiyo sababu itatuchukua kama juma moja, siku kumi au zaidi, kumaliza jambo hilo katika mkutano mmoja, tukiweza. Nafikiri inatosha sana.

5 Sasa, wengi wenu mnasafiri mbali. Ninaangalia nje hapa, nami nimeona tu, muda mfupi uliopita, jamaa wa Tucson. Bibi Sothmann, namwona Ndugu Fred amewasili salama. Nilimwona katika wasikilizaji asubuhi ya leo. Na hapo nafikiri huyo ni Ndugu Don Ruddell anayeketi pale karibu naye huko nyuma, usiku wa leo. Ninafurahi kumwona Ndugu Don akiwa ndani. Na Junior, je Junior yupo hapa, ama yuko kanisani mwake? Nadhani wako kwenye simu kanisani usiku wa leo.

Kwa hiyo, ninyi nyote ndugu, tuna furaha sana kwamba mko hapa pamoja nasi usiku wa leo, na tukimtumainia Bwana kwamba siku moja sisi, wakati siku ya maisha imekwisha na nuru yetu ndogo ya maisha yanayopatikana na mauti inapoanza kufifia na kuzimika, hatutaogopa mabaya yo yote, kwa kuwa chini kote katika ninii—ninii …

6 Nimepata tu ripoti kwenu, huko—kule … huko Arizona, huko Prescott. Ndugu Coggins ameruhusiwa kutoka hospitalini. Kwa hiyo tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo. Vema. Hilo ni sawa. Kwa hiyo tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo. Dada Mercier, baba yako anaendelea vizuri sasa. Nilihisi tu, baada ya sisi kuomba, ya kwamba angekuwa mzima. Kwa hiyo huenda wanasikiliza; Natumaini wanasikiliza; nami nafikiri wanasikiliza. Kwa hiyo tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo, ya kwamba ndugu yetu ni—yuko sawa sasa, na ataendelea kuwa mzima. Kwa hiyo tunamshukuru Bwana kwa mambo haya yote.

Nilikuwa na ombi jana usiku; ndugu mpendwa hapa, nadhani huenda asiwe pamoja nasi leo. Ndugu fulani kutoka huko Kentucky, alinipigia simu kuhusu binti yake. Familia ya kupendeza, na yule—msichana huyo atafanyiwa upasuaji, mama kijana mwenye kansa mgongoni. Kwa hiyo tu—tunaomba ya kwamba Mungu atamkomboa mwanamke huyu kijana. Ninaamini atafanya hivyo, kama tu …

Kusanyiko, sisi sote pamoja, tunaungana na kuwaombea watu hawa, wote pamoja. Hilo ndilo tunalopaswa kufanya, kama kitu kimoja. Kama …

7 Na kadiri siku zinavyozidi kukaribia na kukaribia, na njia kuendelea kuwa nyembamba, tu—tunataka kukaribiana zaidi pamoja. Jamani, hatuna budi kuwa mmoja tu, mwili mmoja. Hatuna budi kusonga pamoja, tukisahau dhambi za mmoja kwa mwingine na tofauti zetu, tukishikamana tu zaidi na zaidi na zaidi, tunapoona Siku hiyo ikikaribia. Kujikusanya pamoja, sote kwa roho mmoja na moyo mmoja. Na kama ndugu, dada akiondoka njiani, kwa njia yo yote, usifanye lo lote ila kumwombea mtu huyo, na kwa upendo, daima tukichukuliana mmoja kwa mwingine. Usi—kamwe usimwache mmoja wenu aondoke. Kaeni pamoja. Na, kama unaweza, ongeza zaidi kwake, daima, wakati wote.

8 Ndugu Neville, nina ombi lako hapa kuhusu Ndugu Wright, Ndugu George Wright anayeketi hapa. Tunafurahi Ndugu Wright na Dada Wright, hapa … Maskini Edith, mimi … Siku moja tutakapokuja, tunataka kuwa na ibada ndogo ya ukumbusho hapa.

Sikurudi kwa ajili ya Edith na wakati alipoenda. Lakini, Dada Wright, unakumbuka ile ndoto aliyokuwa nayo yapata miaka michache iliyopita. Nami niliwaambia wakati huo, nilisema, "Ni, Edith mdogo hatakaa pamoja nasi kwa muda mrefu sana sasa," kwa sababu Bwana alikuwa tayari amewaambia ya kwamba alikuwa akienda, kupitia ndoto ile aliyoota. Nami nikapata tafsiri yake, ilikuwa, ya kwamba alikuwa anaenda kukutana na Mungu. Yapata miaka miwili baadaye, akaenda kumlaki Mungu. Sasa anamngojea baba yake na mama yake wavuke mstari wa kugawanya, kati ya kufa na kutokufa.

Mungu awabariki. Ninataka kujaribu kuwaona mara moja, kama tu ninaweza. Kwa hiyo Mungu awe pamoja nawe na Shelby, na kila mtu. Nilidhani nilimwona Shelby asubuhi ya leo; Sikuwa na hakika.

Huwezi kuona vizuri sana juu hapa; dari imeshuka chini namna hii, na inatupa m—nuru kama hiyo. Unaweza kuona walipo, bali huwezi kuwaona watu vizuri sana.

9 Sasa moja kwa moja kwenye Ujumbe. Huu ni Ujumbe ninaotaka kusoma kutoka Hesabu 19:9 na Waefeso 5:26. Na kama ninyi watu mnaoandika kumbukumbu za somo, na kadhalika, mbona, mnaweza kuliandika.

Na sasa kumbukeni, kama huu unarekodiwa … Sijui. Siwezi kumwona mtu ye yote. Naam, ninamwona, ninamwona Ndugu Terry kule—kwenye chumba cha kurekodi. Na kama haya yananaswa; kwa wahudumu wo wote mahali po pote, wakati wo wote, hili halielekezwi kupuuza mafundisho yenu, hili hata halielekezwi kwa kondoo wenu. Ujumbe huu, na Jumbe zingine zote ninazozungumzia, zimeelekezwa kwa kusanyiko langu. Si kwa kusanyiko lenu isipokuwa wanataka kuupokea. Lakini umeelekezwa kwa watu hawa hapa.

Watu wananunua kanda hizi. Watu kote ulimwenguni wanazinunua na kuzicheza. Mara nyingi wananiandikia. Nami daima ninawaelekeza, kama wao ni washiriki wa kanisa fulani, "Mwone mchungaji wako."

10 Sasa, mchungaji, ninataka ujue jambo hilo, ya kwamba, hili ni kwa ajili ya kusanyiko langu tu ninanena mambo haya. Nami nina haki ya kufanya hivyo, kwa sababu nimewekwa na Roho Mtakatifu kuwachunga kondoo hawa. Na ole wangu kama siwaambii kile ninachofikiri ni Kweli, na jinsi ninavyodhania huja. Lakini si kwa ajili ya ulimwengu wala makanisa mengine. Unafanya kila kitu Mungu anachokwambia ufanye. Siwezi kujibu kwa ajili yenu, wala humwezi kujibu kwa ajili yangu. Lakini hatuna budi kila mmoja kujibu mbele za Mungu, kwa ajili ya huduma yetu. Kwa hiyo, kama itanibidi kuwajibika kwa ajili ya huduma yangu, sina budi kuihubiri kwa njia ambayo ninaiona, kwa njia ambayo imefunuliwa kwangu. Kwa hiyo hebu hilo lijulikane sasa.

11 Sasa katika Hesabu 19:9, tunataka kusoma kifungu hiki, ama Andiko hili, hasa.

> *Na mtu aliye msafi atayakusanya majivu ya huyo ndama, na kuyaweka nje ya marago mahali safi, nayo yatatunzwa kwa ajili ya kusanyiko … (angalia sasa) kwa ajili ya kusanyiko la wana wa Israeli kwa ajili ya maji ya kutenganisha: ni utakaso wa dhambi.*

Angalia, si kwa kila mtu, "kwa kusanyiko la wana wa Israeli; maji ya utengano."

Sasa katika Waefeso, mlango wa 5, na kuanzia kifungu cha 22.

> *Enyi wake, watiini waume zenu, kama kumtii Bwana.*
>
> *Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama vile Kristo alivyo kichwa cha kanisa; naye ni mwokozi wa mwili.*
>
> *Kwa hiyo, kama vile kanisa linavyomtii Kristo, vivyo hivyo wake na wawatii waume zao kwa kila jambo.*
>
> *Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa nafsi yake kwa ajili yake;*

Sasa hili hapa ndilo ninalotaka kusema sasa.

> *Ili apate kulitakasa na kulisafisha kwa maji katika neno,*

12 Sasa, somo hili dogo usiku wa leo, kama ningaliliita somo. Nami ninatumaini ya kwamba watu hapa, na pia huko nje kwenye mawasiliano ya simu, hawatapuuza jambo hili na kufikiri ya kwamba linakusudiwa kwa namna ya kukufuru. Ingawaje, kuchukua somo kama hili, lingesikika la kukufuru. Somo ambalo ninatumia kwa ajili ya usiku wa leo ni: Chujio la Mtu Mwenye Busara. Hilo linasikika ni la kimapinduzi kwa somo, kwa mhudumu ambaye anapinga sana kuvuta sigara, angechukua somo kama hilo, Chujio la Mtu Mwenye Busara. Ilitimia, ya kwamba, hivi majuzi asubuhi nilipokuwa nimeenda kuwinda kindi.

Kama ninyi watu huko nje kwenye—huko nje kwenye redio, hewani, ama kwenye wimbi la simu, mngeweza kuona sura ya kusanyiko hili wakati nilipotangaza somo langu, mngeliweza kutoa kicheko kutokana na hilo. Chujio la Mtu Mwenye Busara.

13 Vema, yote yalitokea ambapo Malaika wa Bwana walinitokea asubuhi moja, na hao kindi walinena wakawa. Ninyi nyote mnakumbuka wakati jambo hilo lilipotukia. Na, pia, kwenye kilele cha kilima nilichokuwa nimesimama, ndipo ambapo … kabla tu ya kuhubiri Nyakati Saba za Kanisa, nikienda kuwinda asubuhi moja kabla ya mapambazuko. Pale walisimama … Nilifikiri jua lilikuwa linachomoza, yapata saa nne asubuhi. Jambo lisilo la kawaida; Niliona Nuru hiyo, nami nikageuka, na pale palisimama Vinara vya Taa Saba vya Dhahabu vikisimama pale juu ya kilima, na kama upinde wa mvua ulikuwa ukija kupitia kwenye mabomba na kulisha.

Mara baada ya hayo, Bwana Yesu alitutokea. Na papo hapo nikasikia Sauti iliyosema, "Yehova wa Agano la Kale ni Yesu wa lile Jipya." Naye alikuwa hapo, baada ya kitambo kidogo, akafunuliwa baada ya vile Vinara vya Taa Saba vya Dhahabu. Basi angalia jambo hilo. Ni wangapi wanaolikumbuka somo hilo? Niliiandika nyuma ya—la sanduku la—la magurudumu niliyokuwa nayo mfukoni mwangu. "Yehova wa Agano la Kale ni Yesu wa lile Jipya." Mungu Mbinguni anajua ya kwamba hilo lilikuwa ni kweli.

14 Nilipovuka mahali pale ambapo Yeye alinitokea baadaye kidogo, kuhusu wale kindi.

Ndipo nilipompigia simu rafiki yangu mzuri, Jack Moore, miezi michache baadaye, kuomba; nilipoanza kuhubiri zile Nyakati Saba za Kanisa, Ufunuo 1. Naye alikuwa amesimama, mweupe mwili mzima; Nywele zake zilikuwa kama sufu. Yeye angewezaje, akiwa bado na umri wa miaka thelathini na mitatu, na awe mweupe mwili mzima? Na Ndugu Moore, mzuri sana, mstaarabu, Mkristo muungwana, na msomi, mmoja wa watu wazuri sana ninaowajua; Naye akasema, "Ndugu Branham, huyo alikuwa ni Yesu baada ya hali Yake ya utukufu. Hivyo ndivyo anavyoonekana sasa." Lakini hilo halikunipigia kengele. Nami nikaendelea kuomba mpaka siku moja …

Kabla sijaanza zile Nyakati Saba za Kanisa, nisingeweza kupata sura hiyo ya 1 vizuri. Mtu angewezaje, mwenye umri wa miaka thelathini na mitatu, aliyefufuka katika mwili ule ule ambao mitume walimtambua, wakamjua kuwa ni; na angewezaje kuwa huko juu, labda mwenye umri wa miaka themanini au tisini, akiwa na sufu kubwa nyeupe juu ya uso Wake, na ndevu Zake nyeupe kama theluji?

15 Nilikuwa nimesoma katika Kitabu cha … cha Danieli, ambapo alimjia "Mzee wa Siku, Ambaye nywele Zake zilikuwa nyeupe kama sufu." Ndipo nikamwona yule Mzee wa Siku. Yeye alikuwa ni yule Mzee wa Siku, yeye yule jana, leo, na hata milele. Unaona, ilikuwa ni mfano, wakati huo.

Kwa nini sufu nyeupe? Na halafu mimi … Roho Mtakatifu alionekana akinena nami juu ya picha niliyoona wakati mmoja, ya hakimu wa kale. Ndipo nikaenda kwenye historia; Nilirudi katika historia ya Biblia na yote, kujua. Nao mahakimu wa kale, kama vile kuhani mkuu katika Israeli, ilimbidi kuwa na hizo nywele nyeupe, nywele na ndevu zenye mvi, kwa sababu zile nyeupe juu yake zilionyesha kwamba yeye alikuwa ndiye mamlaka kuu ya mahakimu katika Israeli.

Na hata katika siku hizi, na hadi miaka mia chache iliyopita, labda miaka mia kadha iliyopita, ama labda si hivyo, baadaye kuliko hapo. Majaji wote wa Kiingereza, haidhuru walikuwa ni vijana vipi au walikuwa na umri gani, walipoingia kwa ajili ya hukumu, walivaa wigi nyeupe; na kuonyesha ya kwamba hakuna mamlaka mengine, katika ufalme huo, juu ya neno lao. Neno lao ndilo la mwisho la huo ufalme. Kile wanachosema, ni hicho tu.

Na sasa, basi, niliona jambo hilo. Huyo hapo alikuwa amesimama pale, bado ni Kijana, lakini amevaa wigi nyeupe. Yeye alikuwa ndiye Mamlaka yote, kamilifu. Yeye alikuwa Neno. Naye anafanya hivyo, amevaa wigi nyeupe.

16 Halafu, baadaye tulipomaliza, na ma—mahubiri, na tukaenda magharibi, na wakati Malaika wa Bwana walipojitokeza kule nje kwa ajili ya ile Mihuri Saba, nayo ikaenda hewani (ambayo tuna picha yake hapa, na kila mahali nchini), huyo hapo alikuwa amesimama pale, angali amevalia wig pamoja na mamlaka hayo makuu. Yeye ni Kichwa cha Kanisa. Yeye ni Kichwa cha Mwili. Hakuna kitu kama Yeye, mahali popote. "Yeye aliumba vitu vyote kwa nafsi Yake. Yeye aliumba vitu vyote kwa ajili Yake, na pasipo Yeye hakukuwa na kitu kilichoumbwa." "Yeye ana mamlaka yote Mbinguni na duniani," na kila kitu ni mali Yake. "Na katika Yeye unakaa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili." "Naye Neno alikuwa Mungu, naye amefanyika mwili miongoni mwetu." Naye alikuwa Ndiye aliyefunua siri yote ya mpango wote wa wokovu, ambao manabii wote na watu wenye hekima walikuwa wamenena habari zake. Yeye pekee ndiye aliyekuwa na wigi na mamlaka kuu.

17 Sasa, nilikuwa nimesimama, huko juu kilimani asubuhi nyingine, ilionekana kana kwamba kulikuwa na kindi waliokuwa wakikata kule juu. Nami nikaanza kuketi. Nami nimekuwa tu pale kwa muda mfupi, wakati, vichaka vilipigwa na mimi, na jamaa fulani mkubwa sana mwenye namna ya bunduki yenye mitutu miwili akaja akitembea vichakani kule, na kama kwamba alinitisha kiasi cha kufa. Nikaenda kule, nikainama chini; Niliogopa kusogea, nilihofu angenipiga risasi. Na vichaka vikitembea, kwa hiyo nilikaa kimya kabisa.

Kindi akaanza kupanda juu ya kilima, naye akafyatua risasi kwa mitutu yake mwili. Na kwa hiyo akamkosa, na kwa hiyo kindi akashuka juu ya kilima. Nikawaza, "Sasa nitaondoka; kelele yote hiyo inatoa mwangi. Alikuwa na bunduki yake ikiwa haina risasi."

Nami nikaanza kushuka kilimani, na jamaa huyo akapiga risasi moja kwa moja mbele yangu. Ilinigeuza nyuma namna hii. Nami nikaanza kuja hapa, kushuka kwenda upande mwingine, na bunduki ya ishirini na mbili ikaanza kupiga risasi, na risasi zikivuma juu yangu. Nikasema, "Aisee, niko mahali pabaya sana."

18 Kwa hiyo nikageuka nikaenda karibu na mto. Nami nikawaza, "Nitashuka niende hapa chini na kujificha mpaka watakapomaliza, kusudi niweze kutoka." Na nilipokuwa nikishuka chini, ilitokea kuvuta … Usikivu wangu ulivutwa kuangalia upande wangu wa kulia. Na, kama nilivyofanya, kulikuwako na pakiti tupu ya sigara ambapo mmoja wao alikuwa ameitupa chini, katika mbio zote za … wakati kindi walipokuwa wakipita vichakani.

Nami nikachukua pakiti hii fulani ya sigara, nami nikaangalia … Sikuichukua kamwe; Naomba msamaha. Niliitazama hapo chini. Sikuikokota, maana sipendi harufu ya vitu hivyo, kwa kuanzia. Nami nikaangalia kule chini, na ni—ni kampuni fulani ya tumbaku ambayo nadhani sipaswi kutaja jina lao, bali

mtajua. Ilisema pale, "Chujio la mtu mwenye busara na ladha ya mtu anayevuta sigara."

Nikaangalia kitu hicho, na nikawaza, "Chujio la mtu mwenye busara?" Nikawaza, "Kama mtu huyo angeweza kuwazia hata kidogo, asingevuta sigara hata kidogo. Ingewezaje kuwa 'chujio la mtu mwenye busara'? Mtu mwenye busara hangevuta sigara hata kidogo." Vema.

19 Sasa, niliwazia, "Huo ni udanganyifu iliyoje!" Sasa, hayo makampuni ya tumbaku yanapaswa kuwa ya Marekani. Na loo, kama tukiishi kulingana na sera zetu, tungekuwa tunafanya kazi kusaidiana mmoja kwa mwingine, kama tuna hisia mmoja kwa mwingine. Na jinsi ulivyo unafiki! Sababu ya mimi kutokuita jina la kampuni hiyo, sina budi kusema mambo mabaya juu yao. Na mtu yeyote anawezaje kuwa mnafiki, kupata pesa?

Mtu mwenye busara hatavuta sigara hata kidogo. Lakini jinsi umma wa Marekani unavyodanganyika kwa hilo; wanafikiri ya kwamba hilo ni zuri sana!

Sasa angalia, huwezi, huwezi … Mwulize mtu ye yote, wanasayansi, mtaninii … Huwezi kuwa na moshi bila kuwa na lami. Kama kuna chembe moja ndogo ya moshi inayopitia, hiyo ni lami. Na kama hupati moshi wowote, vema, hupati lami yo yote, wala hupati cho chote kile. Unachora tu dhidi ya fimbo imara. Lakini mradi tu unapata moshi wowote, unavuta kansa, nikotini.

20 Kama ungalikuwa pamoja nami mwaka jana, ama mwaka uliopita, naamini ilikuwa, kwenye Maonyesho ya Ulimwengu, wakati Yul Brynner na hao wote walipokuwa kule kwenye maonesho, na unawaona wakichukua sigara hiyo, wakiiweka katika kitu fulani, na kuivuta kwenye kipande cha marumaru. Na huyo daktari akichukua pamba, akavingirisha pale na kutoa nikotini kutoka kwake, na kuiweka mgongoni mwa panya mweupe, na kumweka kwenye kizimba. Na kila siku saba walimtoa nje. Na yule panya alikuwa amejaa saratani sana asingeweza kutembea, kutoka kwenye nikotini kutoka kwenye sigara moja.

Ndipo akasema, "Unajua, wanasema ya kwamba unaweza kuipata kupitia chujio." Yeye alisema, "Huwezi kuwa na chujio … Chujio lo lote linaloweza kutoa nikotini, linatoa moshi," kasema,"kwa sababu huna budi kuwa na moshi … uwe na lami kutengeneza moshi, na ni lami inayotoa saratani."

Ndipo basi akaenda, akaivuta kupitia kwenye maji, na kusema, "Wakati mwingine unafikiri ungeweza kuichuja." Kasema, "Kila wakati, hiyo, haijalishi unaivuta wapi." Kasema, "Wanasema, 'Mimi siivuta pumzi,' kisha wanaiweka mdomoni mwao na kuitema." Ndipo akachukua hiyo na kuikunja, na kuiweka chini ya kitu fulani pale, na akaonyesha bado ilikuwa ni saratani. Unafanya nini? Kuimeza moja kwa moja kwenye koo lako. Mnaona? Na haidhuru unafanya nini, bado ni mauti. Mnaona?

21 Na halafu kuwazia ya kwamba kampuni ingemdanganya mtu vya kutosha, ama kujaribu kuwadanganya watu wao wenyewe. Ni kama tai anayeishi kwa aina yake, kwa namna yake. Kutafuta pesa, kuuza mauti kwa—nchi, na kwa vijana wa kiume. Na kwenda huko nje kwenye uwanja wa vita na kuwafia, kisha wageuke na kuuza kitu kama hicho, chini ya kujifanya bandia, "Chujio la mtu mwenye busara, bali ladha ya mtu anayevuta sigara." Ni lazima kuwa na moshi kupate ladha. "Ladha ya mtu anayevuta sigara."

Jinsi watu wanavyodanganyika kwa hilo, hata hivyo! Wanalipata. Sasa, ni kuwadanganya tu zaidi. Unaona, ni la ibilisi. Hawajali maisha yako. Hawana huruma kwa ajili yako. Wanakuuzia kitu hicho ili tu wakuangalie ukifa, mradi tu wanapata pesa.

22 Kama vile siasa na vita. Siamini katika vita. Siamini ya kwamba sisi sote tungepaswa kuwa na vita.

Ninaamini katika Ufalme mkuu ambao Mungu anauleta, ustaarabu mkuu ambao utashushwa chini ya utawala Wake Mwenyewe ulio mkuu; hakutakuwa na vita vingine kamwe. Taifa halitainua mikuki dhidi ya mataifa. Wote watakuwa ni amani, amani ya Milele.

Kwa hiyo ustaarabu wa namna hii unaleta vita. Na kadri tunavyokuwa wastaarabu zaidi, chini ya huu, ndivyo tunavyozidi kuwa na vita. Mmoja akijaribu kuwa mstaarabu zaidi kuliko huyo mwingine, na kadri unavyostaarabika zaidi hufanya vita zaidi. Mnaona?

Na angalia ni nini, chini ya ustaarabu huu, kwamba mtu angetoa kitu kama hicho. Na jambo pekee kinachofanya, kinakudanganya tu kukufanya ununue sigara zaidi. Kwa maana kama mtu akivuta sigara … Nami ninaamini ni ya ibilisi, na kuna pepo wa nikotini katika mwanamume na, ama mwanamke. Na kama sigara moja ikimridhisha huyo pepo wa nikotini hata atakuacha peke yako na kuacha kukusumbua, kwa sigara moja. Na halafu unachukua chujio, unaachilia tu theluthi moja ya moshi huo upite hapo, ama theluthi moja ya hiyo nikotini ipitie pale, ndipo itahitaji sigara tatu kuchukua mahali pa hiyo, nawe utavuta moshi tatu kwa mmoja.

Unaona, ni tu—ni hila, udanganyifu, hila ya kujaribu kuuza sigara. Wanaweza kuuza zaidi kwa njia hiyo kuliko wanavyoweza kwa kumwacha tu mtu avute sigara moja kwa moja kwenye kiko chake au kwenye sigara yake. Sasa, unaona, ni ya ibilisi.

23 Nilipokuwa nimesimama pale nikiliangalia, na kuwazia jinsi lilivyokuwa la udanganyifu, swali lilinijia. Nami niliinama tena, nikaangalia pakiti hiyo tena, nami … ilionekana tu kama kitu fulani kiliniambia, "Lakini ule msemo ni sawa, 'chujio la mtu mwenye busara, ladha ya mtu anayevuta sigara.'" Ilinijia ya kwamba udanganyifu huo, pia, katika ulimwengu wa kawaida kule kwenye tumbaku, ni kitu fulani kwa utaratibu wa makanisa ya siku hizi, unaona, udanganyifu.

Imekuja mpaka ulimwengu mzima umekuwa udanganyifu mkuu wa kile kilicho kweli halisi na kilicho sahihi. Mnaona, hata katika siasa, na katika mambo ya kijamii, shuleni, katika kila kitu, inakuwa udanganyifu.

24 Kijana mmoja alikuwa akiniambia hivi majuzi ya kwamba alikuwa ameshuka kwenda kwenye kambi ya jeshi, na askari kijana alikanyagwa na kifaru; mapafu yake, tumbo lake, ama cho chote kile, alipasuliwa. Nao wakaenda hospitalini; walikuwa na madaktari watatu ama wanne wamesimama pale kwenye mstari, na kila mtu amesimama kwenye mstari. Na askari wawili au watatu wakiwa wamemshika rafiki yao, naye alikuwa vigumu kupumua … Kila wakati alipopumua, ubavu huo ungemchoma moja kwa moja kwenye mapafu yake, na hilo lingemfanya kutokwa na damu kwa ndani. Nao wakamwacha huyo kijana mwanamume asimame pale kwenye mstari huo, huko nyuma kabisa ya mstari, na kuwaacha, baadhi ya hao jamaa wasio na kitu ila kuumwa na sikio ama kitu fulani, waendelee.

Na yapata wakati alipofika kule juu, kanali fulani akaja na mtoto mdogo aliyekuwa na vipele, mvulana wake mdogo ama msichana alikuwa na vipele mkononi mwake. Nao wakausimamisha ule mstari, kumwingiza mtoto wa kanali, na mvulana huyo ametobolewa, akiwa anakufa. Haya basi.

Loo, kama kanali huyo angalikuwa na hisia za kweli kwa ndugu yake huko nje kwenye mstari, angesema, "Mtoto huyu anaweza kungojea. Mlete mtu huyo hapa upesi, fanyeni jambo fulani kwa ajili ake!"

25 Lakini kila mtu anataka kuonyesha mamlaka yake. Sasa, wote si hivyo; la, wote hawako hivyo. Lakini kuna mengi mno kama hao. Kuna wengi mno ambao wako hivyo. Lakini mtu huyo, jambo pekee alilokuwa akiwazia, alikuwa ni mvulana wake mdogo aliyekuwa na vipele mkononi mwake, na bila kuwazia juu ya yule maskini mvulana aliyesimama pale amepondwa na kifaru, kifaru kile kile na labda mvulana yule ambaye angeokoa maisha siku moja kwenye uwanja wa vita. Mnaona, hawaachi kuwaza; ni kwa ajili yao tu.

"Chujio la mtu mwenye busara."

Nilitazama kitu hicho, na nikawaza, "Ni kitu kama ma—madhehebu ya siku hizi, makanisa tuliyo nayo." Kila mmoja wao ana chujio lake; wana aina yao ya chujio. Yanaachilia tu kile yanachotaka kiingia, na kile kisichoingia; yale yanayoyachuja kuingia na yanayochuja yasiingie , kwa chujio la aina yao yenyewe. Yanaacha tu kiasi fulani cha ulimwengu kuingia kuwaridhisha wasioamini walio mle ndani. Yatawaingiza ndani haidhuru wao ni akina nani, kama wana pesa. Yatawaingiza ndani haidhuru wao ni nani, kama wanapendwa na watu.

Lakini kuna jambo moja juu yake, huwezi kuingia katika Kanisa la Mungu namna hiyo; si madhehebu sasa, ninamaanisha Kanisa halisi, kanisa halisi la Mungu.

26 Kama vile makampuni ya tumbaku ya siku hizi, watu wanaoingia kwenye haya makanisa yaliyosemwa ama madhehebu, wana ladha, na ladha hiyo ni yaliyobora ya ulimwengu. Na kila dhehebu lina chujio lao wenyewe, nao wanawachuja Wakristo wote wa kweli ambao wangesema "amina" wakati alipokuwa akihubiri; na kuwaingiza Mayezebeli wote waliokata nywele zao, waliopakwa rangi walio nchini, mradi tu ni watu maarufu. "Fulani na fulani anakuja kwa … mwigizaji maarufu wa sinema, mtu mashuhuri." Hiyo ndiyo aina ya chujio wanalotumia. "Madhehebu yetu. Fulani na fulani, rais, ama yule—ama kanali, ama mtu fulani ni mfuasi wa dhehebu letu." Mnaona ni aina gani ya chujio wanayotumia? Chujio hilo, bila shaka, ni la ulimwengu, watu wa ulimwengu.

Watu, wanajua wanachotaka. Kwa hiyo kama itawabidi kupata wanachotaka, basi itawabidi kuwa na chujio la namna fulani, na ulimwengu wa kutosha kuzungumza, kuridhisha ladha yao ya kilimwengu. "Chujio la mtu mwenye busara, ladha ya mtu anayevuta sigara." Chujio la ulimwengu wa kidini, na ladha ya mtu wa kilimwengu.

27 Wanataka kuwa wa kidini. Wanafikiri hawana budi kuwa wa kidini, kwa sababu wana nafsi.

Tulipokuja kwa mara ya kwanza nchini humu, mlikuta Wahindi wakiabudu jua na kadhalika, kwa sababu (kwa nini?) Yeye ni mwanadamu. Tunarudi kwenye misitu ya mbali ya Afrika, tunawakuta wenyeji wakiabudu kitu fulani. Kwa nini? Wao ni wanadamu, nao wanataka, hawana budi kuabudu.

Kwa hiyo mwanadamu, haijalishi ameanguka namna gani, angali anajua kuna kitu fulani mahali fulani. Lakini yeye ana ladha hiyo ya ulimwengu, hata hawezi kuchukua chujio sahihi. Hana budi kuwa na chujio alilojitengenezea mwenyewe. Kila mmoja akifanya chujio la aina yake.

Kila kampuni ya sigara inajivunia yao, yale wanayoweza kufanya, "Chujio halisi! Hii ndiyo chujio bora zaidi! Wote wako mbele!" na wote namna hiyo. Kasema, "Ladha huja," ama kitu fulani, "kutoka mbele." Loo, kwa ajili ya wema. "Mbele"? Kuna nini nyuma yake, hata hivyo? Hakika si mwanamume mwenye busara wala mwanamke mwenye busara. Lakini hivyo ndivyo wanavyosema, kuwadanganya tu watu.

28 Sasa tunaona, ya siku zetu, ya kwamba watu wana ladha. Na kwa nini mwanaume huvuta sigara? Ni kutosheleza ladha. Mwanamke huvuta sigara kwa nini? Kutosheleza ladha.

Na halafu kama kanisa limefikiria, kundi la kidini, wao … kuwaingiza watu mle, hawana budi kuwa na chujio la namna fulani kuwapa watu ladha wanayotaka. Kwa hiyo kama hawapati ladha yo yote watakayo, hawataki sigara. Na kama hawawezi kupata ladha wanayotaka katika dini, hawachukui dini. Sasa, ni dhahiri tu iwezavyo kuwa.

Wanawake wenye kaptura, nywele zilizokatwa, nyuso zilizopakwa rangi, wamevalia mavazi ya kizinifu, wanataka jambo hilo. Wanapenda jambo hilo.

Kama nilivyonena asubuhi ya leo na Jumapili iliyopita asubuhi, juu ya gurudumu hilo katikati ya gurudumu, ama ile nafsi ndogo ya ndani iliyo ndani ya roho. Jinsi ambavyo roho aliye nje, kati ya nafsi na mwili, anaweza kutiwa mafuta kabisa na Roho Mtakatifu. Je! Nyote mlielewa jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.]

29 Sasa kuifuata hiyo pamoja na mwendelezo wa Ujumbe, Mungu Wa Ulimwengu Huu, Watiwa Mafuta Katika Siku Za Mwisho. Huo wa nje, duara wa katikati … Mzunguko wa kwanza ni—ni hisi za mwanadamu. Mzunguko wa pili ni hisi za roho; mapenzi, mapenzi ya kibinafsi, tamaa, na kadhalika. Lakini ndani ni nafsi; nafsi hiyo ilichaguliwa tangu awali.

Kwa hiyo, wanaweza kuitia upako roho hii kuufanya mwili wa nje kuja chini ya utawala wa roho. "Bali nafsi itendayo dhambi, hiyo nafsi itakufa." Nafsi inayolikataa, katika kutokuamini, Neno la Mungu, ambalo ni sehemu yake, nafsi hiyo itaninii Milele … imekuwa, daima.

Ninaamini katika mauti ya Milele, kama vile ninavyoamini Mbingu ya Milele, bali si kuzimu ya Milele. Hakuna kitu kama kuzimu ya Milele. Kuna mauti ya Milele kwa watu ambao ni … Wengi wao, wa kidini, ulimwenguni leo, daima wamekufa.

"Mwanamke anayeishi katika anasa," akiwa na nywele zilizokatwa na uso wake uliopakwa rangi, "amekufa angali hai." Biblia ilisema hivyo. Mnaona? Unaona, huenda yeye ni wa kidini, bali kamwe hakuokoka. Yeye ana msisimko wa nje. Huenda akaimba katika kwaya, ama huenda akacheza katika Roho, huenda akanena kwa lugha, na kuwa na madhihirisho yote ya Roho. Lakini isipokuwa nafsi hiyo iliyo ndani ni binti ya Mungu, mnaona, yeye ameondoka, haidhuru anafanya nini.

30 Israeli wote walikuwa wa kiroho kwa nje, wote walijazwa na wema wa Mungu, na jinsi walivyomheshimu Mungu, na kadhalika, lakini hilo halikufanya kazi. Ndani yao hawkuweza kulitambua Neno Lenyewe.

Lakini wakati unapozaliwa na Roho wa Mungu, basi una ninii … wewe ni mwana wa Mungu, na daima ulikuwa mwana wa Mungu, na daima utakuwa mwana wa Mungu. Hakuna njia ya kuutenganisha, kwa sababu ni … una Uzima wa Milele. Na Milele kamwe haikuanza; wala haitakwisha kamwe.

31 Loo, kwa ajili ya neema ya Mungu, kwamba angetupa ufahamu wa siri hizo kuu! Kama vile Paulo alivyonena hapa, chini zaidi katika Waefeso, akinena juu ya mume na mke, na kusema, "Hii ni siri," jinsi wanawake wanavyopaswa kuwaheshimu waume zao. Hata nafasi ya pili, ninaamini ni, Biblia nzima, ambapo heshima ilipata kuzungumziwa. Kasema, "Wanawake, wakiona anamheshimu mumewe, wanamheshimu mumewe." Ndipo mume anapaswa kuishi maisha kama hayo mbele ya mkewe hata mkewe aweze kumheshimu kama mwana wa Mungu. Na kama yeye haishi maisha ya namna hiyo, vema, basi, bila shaka, asingemheshimu, kwa sababu anajua kile yeye alichofanywa nacho. Lakini wakati ni mwanamume aliye mcha Mungu, mwenye kicho na msafi, pamoja na mke wake na mbele ya familia yake, mtumishi halisi wa Mungu, basi wanawake, watoto, na wote, wanapaswa kumheshimu mtumishi huyo wa Mungu, kwa kicho.

32 Angalia sasa. Mwanamke, wanataka kuwa na nywele zilizokatwa. Wanataka kuvaa kaptura, kujipaka rangi, kujipodoa. Hizi bikini ndogo na kadhalika ambazo wao—ambazo wanavaa siku hizi, wanataka kufanya hivyo; na hata hivyo wanataka kwenda kanisani. Mnaona huo upako juu ya roho, si juu ya nafsi. Mnaona?

Kasema, anataka kuwa Mkristo na pia kufanya mambo haya, na mchungaji anasema ni sawa. Ndipo kama akisema ni sawa, "Unaweza kuwa mshiriki; jina lako linaweza kuwa kwenye kitabu changu cha kanisa hapa; ni sawa," basi anampa chujio lake la kimadhehebu kuendana na ladha ya mwanamke wa kilimwengu. Anaupenda ulimwengu; anapenda ladha yake. Kwa hiyo ana chujio kwa ajili yake, bali yeye yuko mbali sana na kuwa mwanamke mwenye busara. Lakini haya basi. Hapo ndipo nilipolipata somo hili.

La, yeye si m—mwanamke mwenye busara. Kama alikuwa na busara, angejua kanisa halitamhukumu kwenye Siku ya mwisho. Kanisa linamhukumu sasa kwa ushirika wake, uaminifu wake kwa makundi ambayo yeye ni mfuasi wake na vyama. Wanamhukumu sasa kwa jambo hilo. Lakini Mungu atamhukumu kwenye Siku ya mwisho. Kwa hiyo yeye hafikirii.

33 Ni kama tu mtu anayevuta sigara; yeye anaipenda sigara vizuri sana mpaka nguvu zake za kufikiri zimefa ganzi kwa nikotini. Na tamaa za mwanamke huyo zimeziba nguvu zake za kufikiri mpaka atafanya mambo haya yaliyo maovu machoni pa Bwana, maana anataka kufanya hivyo; linatosheleza ladha ya mwanamke wa kilimwengu. Kwa hiyo anachukua chujio la kanisa la kilimwengu; yeye anaipitia moja kwa moja, vema, hakuna cha kumsumbua. Huonyesha …

Sasa tunaona pale ya kwamba hiyo ni Kweli. Naye mchungaji anasema, "Hilo ni sawa kabisa. Hatuhukumu wanawake kwa kufanya hivyo. Ni sawa kabisa." Kuna dhambi ya kutosha ndani yake; hiyo ni kupitia chujio lake. Inaonyesha ya kwamba walipitia chujio la kitheolojia. Nao wana ladha ya kitheolojia; nao walikuwa na ladha ya kitheolojia. Lakini hakika haikupitia katika Chujio la Mungu. La, bwana.

34 Sasa, kama kuna chujio la kitheolojia kwa mwenye mawazo ya kitheolojia, na kuna chujio la kanisa kwa ajili ya mwenye mawazo ya kanisa, chujio la sigara kwa ajili ya mwenye mawazo ya sigara, hapana budi kuwe na chujio halisi mahali fulani kwa ajili ya mwenye mawazo halisi. Na Mungu ana Chujio, na hilo ni Neno Lake. Ni utenganisho, kwa kuwa ni maji ya utengano kwa ajili ya dhambi. Sasa, huyo ni mtu mwenye busara au ladha ya mtu mtakatifu.

Na kama mtu anapitia chujio la namna hii la ulimwengu, yeye—yeye ana ladha ya kilimwengu. Na kama kampuni ya tumbaku, yeye hupata washiriki wengi kanisani mwake kwa kuwasukuma kupitia kwenye chujio hili. Kama wakisema, "Kuna wanawake wengi zaidi wanaoenda kanisani kuliko wanaume." Hilo linaweza kuwa hivyo. Sasa, hiyo huenda ikawa ni kweli kabisa, wakati anapoweza kwenda na kufanya lo lote analotaka kufanya. Hiyo ni kweli. Atafanya hivyo, atajiunga na chochote, bali alipitia kwenye chujio hilo la kanisa. Kama angepitia kwenye Chujio la Mungu, angekuja tofauti na hilo. Mnaona? Asingeweza kupitia kwenye Chujio la Mungu na kutoka akiwa na nywele zilizokatwa. Hawezi tu kufanya hivyo.

35 Sasa hili litakuwa ni la—lenye uchungu kidogo labda kwa mtu fulani. Lakini wakati alipoanza kupitia kwenye Chujio la Mungu, na linasema mle ndani wao wasikate nywele zao, basi (nini?) Anakaa ng'ambo ya pili. Kama ilisema ni dhambi kwa mwanamke kufanya jambo kama hilo, naye ni aibu kufanya hivyo.

"Kama akitaka," husema, "vema, hana budi kukatwa nywele zake."

Kasema, basi, "Unyoe basi." Kisha akasema, "Tunajua ya kwamba hiyo ni aibu kwa mwanamke kunyolewa nywele." Kasema, "Basi na afunikwe kichwa chake." Na nywele zake ndizo kifuniko chake; si kofia, mama. Nywele zake ndizo kifuniko chake, Biblia ilisema. Sawa. Inaonyesha yeye ni Mnadhiri kwa Bwana. Nywele ndefu, kwa mwanamke, zinamaanisha Mnadhiri kwa Bwana. Sasa, tunaona ya kwamba hiyo ni kweli.

Lakini tunaona kama mtu mwenye busara, anayeitwa hivyo ulimwenguni, anaweza kuvuta sigara na bado apate ladha yake, anapaswa kuwa na akili ya kutosha kujua anapata lami kutoka kwenye tumbaku. Lakini ni kwamba tu, kile imefanya, ni kumuuza zaidi, kumfanya anunue sigara zaidi.

36 Na chujio la kanisa hupata ushirika na mambo kama hayo wanapowaacha wafanye chochote na wangali ni wafuasi wa kanisa, wanapata washiriki wengi zaidi. Vipi kama tungeenda makanisani usiku wa leo na kumchuja kila mtu mbali na hao waliokuwa Wakristo halisi waliozaliwa kwa Neno. Kungekuwa na mahubiri mengi matupu juu ya ukuta usiku wa leo, ni kweli, maana yalipitia kwenye Chujio.

Na kama nina shauku moja moyoni mwangu, nami natumaini ya kwamba kila mtu anayenisikiliza ana jambo lile lile, "Mungu, nipitishe katika Chujio Lako." Kama vile Daudi alivyosema, "Nijaribu, na unipime, uone kama kuna uovu wowote ndani yangu, basi uondoe, Bwana." Mnaona? Ninataka Chujio la Mungu. Sijali kile ulimwengu unachofanya, kile kanisa lilicho nacho; Ninataka kuwa mtu mwenye busara, kuwazia ni Nani nitakayesimama karibu naye moja ya siku hizi, kwa ajili ya Hukumu.

37 Angalia, kampuni ya tumbaku hufanya hivyo ili kuuza sigara zaidi; kanisa hufanya hivyo ili kupata washiriki wengi zaidi. Mwanamke mwenye nywele fupi, akivaa kaptura, angekwama katika Chujio la Mungu. Asingeweza kuipitia, akiwa na nywele fupi, kwa sababu Biblia ilisema hapaswi kufanya hivyo. Yeye huaibisha kichwa chake anapofanya jambo hilo. Tunapaswa kujua jambo hilo. Lakini yeye anapitia moja kwa moja kanisani vizuri, hao wengine wote. Ninasimama wakati mwingine …

Siyo Kutomjali mtu ye yote; Kamwe sisemi kibinafsi juu ya mtu ye yote, bali ni dhambi kanisani. Ninyi mnanishuhudia juu ya jambo hilo. Sikusema, "Bibi Fulani na fulani ni fulani na fulani, au Bw. Fulani na fulani, ama Kasisi Fulani na fulani ni fulani na fulani." La, bwana. Nasema dhambi ni dhambi. Kama liko katika familia yangu, liko ndani yangu, liko ndani ya ye yote yule, bado ni dhambi. Si kama mtu binafsi, sizungumzi dhidi ya watu binafsi. Ninanena dhidi ya dhambi. Sijali kama ni mimi ama ye yote yule, inaanza

kupitia kwenye Chujio la Mungu, dhambi yoyote itakuzuia papo hapo.

38 Angalia. Lakini mwanamke anayetaka kuwa na nywele fupi na kuvaa kaptura, ama kuvaa rangi na chochote kile, yeye anaweza kupitia moja kwa moja chujio la Kipentekoste kwa urahisi tu kama sambusa, hakuna kitu juu yake, moja kwa moja hata mautini. Maana, yeye ninii … Yeye anasema, "Vema, hakuna ubaya katika jambo hilo."

"Ukiipenda dunia au mambo ya ulimwengu, ni kwa sababu kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako."

Huko chini kupitia katika roho hii, basi, anaweza kuvuta ndani ya nafsi yake, mambo ambayo si ya Mungu na dhidi ya Neno la Mungu, kama hiyo ndiyo ladha katika nafsi. Inaweza kuja kupitia ladha; unaona, ladha … Inaweza kuja kupitia katika kufikiri, kupitia hoja, "Hakuna ubaya ndani yake. Nina ladha. Nina hisia. Ninajisikia ya kwamba hii ni sawa." Anaweza kuja moja kwa moja kupitia kwenye jambo hilo, na kuingia moja kwa moja kwenye nafsi yake, kama nafsi yake ni ya aina hiyo. Inaonyesha ya kwamba yeye havutii kupitia Chujio la Mungu.

Lakini kama ana nywele zilizokatwa, amejipodoa, kaptura, suruali, anafanana na mwanamume, suruali hizi zote na cho chote wanachowaita; akisema mambo ya namna hiyo, na kufanya mambo hayo, na kuishi kwa ajili ya ulimwengu, atakoma; hawezi kupita kule. La, bwana. Itamzuia hapo mwanzo.

39 Angalia, mwanamume akiangalia midomo yake myekundu sana na uso uliopakwa rangi, na kaptura na —na bikini, na chochote alicho nacho; mtu mwenye busara kabisa hatamwangalia. Sasa, mwanamume ambaye ni mfuasi wa kanisa atamwangalia, ampende. Lakini sijali jinsi anavyoonekana kwa macho, mwanamume mwenye busara atageuza kichwa chake. Kwa nini? Yeye amepitia kwenye Chujio la Mungu, naye anajua kumtazama ni uzinzi moyoni mwake. Yeye hawazii kuwa ni mrembo.

Sema, "Je! Yeye si kitu kizuri!"

Si kwake si hivyo. Yeye ni mwonekano mchafu, Yezebeli mwenye mashaka mchafu, kwa mtu mwenye busara. Mwana wa Mungu anamwangalia kwa aibu kwamba hata yeye ni wa familia yake. Hiyo ni kweli. "Huyo angewezaje kuwa dada yangu na kutenda hivyo?"

Mnaona, yeye alipenyeza kwenye chujio moja, naye akapitia kwenye lingine. Yeye hatafikiri yeye ni mrembo, hata kidogo. Huo si uzuri kwa mtu halisi wa Mungu.

40 Kumbukeni, wakati mmoja kabla ya Damu ya Yesu Kristo kuwa Chujio, kama tutakavyofikia katika dakika chache, "Wana wa Mungu waliwaangalia binti za wanadamu, ya kwamba ni wazuri, wakajitwalia wake." Mungu kamwe hakusamehe jambo hilo. Tena ilitukia, katika safari ya Israeli, na Mungu kamwe hakuwasamehe. Kila mmoja wao aliangamia.

Chujio la mtu mwenye busara!

Ninatoka mkutanoni hapa; kulikuwako na ricky kidogo akisimama hapa nyuma ya kanisa usiku mmoja, akaniambia, yapata miaka mitatu ama minne iliyopita, kasema, "Sababu ya kusema hivyo, wewe ni mzee." Kasema, "Nafikiri wanaonekana wazuri."

Nikasema, "Ninaweza kuwazia jambo hilo." Kwa sura yake tu, unaweza kujua jinsi alivyoonekana. Nikasema, "Hebu niwaambie jambo fulani. Una umri gani?"

"Yapata umri wa miaka thelathini."

Nikasema, "Nilipokuwa mdogo kwako kwa miaka kumi na mitano, niliwazia jambo lile lile." Sawa. Na bado ni uchafu!

41 Chujio la mtu mwenye busara! Sasa angalieni, kama amekuwa, akili yake imechujwa kupitia Neno la Mungu, Chujio la Mungu, hatamwangalia mwanamke huyo. Yeye hatadhani ni mrembo; atafikiri yeye ni Yezebeli. Atafikiri, nyuma ya midomo hiyo myekundu kuna meno ya sumu ambayo yangemchoma. Na Biblia ilisema, "Malango yake ni malango ya kuzimu; na mtu akiingia ndani yake ni kama ng'ombe akienda machinjioni mwake." Kuna Chujio la mtu mwenye busara.

Unatamani nini? Wakati mwanamke huyo anaposhuka kuja barabarani amevaa hivyo, nawe mwanamume unageuza kichwa chako, ukiangalia kote namna hiyo, hutumii Chujio la mtu mwenye busara. Kwa sababu, unapofanya jambo hilo, unafanya uzinzi, kwa kuwa Chujio lilisema, "Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye." Geuza kichwa chako, mtu mwenye busara. Ondokeni kwake. Yeye si mrembo. Yeye ni nyoka; hiyo ni kweli, anajisokota kama nyoka, anatenda kama nyoka, anagonga kama nyoka. Kaa mbali naye.

42 Loo, naam, Neno la Mungu ni Chujio la mtu mwenye busara. Kila mtu anajua jambo hilo. Hivyo ndivyo nafsi yako inavyochujwa, na Neno la Mungu. Na Linafanya, unapokuja kupitia kwa Mungu … Wakati mtu

mwenye busara anapopitia kwenye Chujio la Mungu, linampa ladha ya mtu mtakatifu. Hiyo ni kweli. Unapopitia kwenye Chujio la Mungu, basi ladha yako ni ladha ya mtu mtakatifu. Hufanya ladha ya mtu mwenye haki. Kauli mbiu hiyo hakika ni sawa.

Sasa tunaona jinsi jambo hili lilivyofanywa kwa mfano, katika Israeli, kwa ajili ya kusanyiko la Israeli pekee. Hiyo ndiyo sababu, tukinena jambo hili sasa, kama wahudumu hawakubaliani juu ya jambo lolote lililosemwa; Hili ni kwa ajili ya kusanyiko langu ambalo Bwana amenipa ku—kulihubiria.

43 Angalia katika Kutoka 19, nawatakeni msome mnapoenda nyumbani, mtakapokuwa na wakati zaidi. Angalia, wakati Israeli walipokuwa wamefanya dhambi, kwanza walimchukua ndama mwekundu ambaye kamwe hakuwa amewekwa nira shingoni mwake. Hiyo inamaanisha kamwe hakufungwa nira na chochote.

Naye ilimbidi awe mwekundu. Rangi nyekundu ni—ni rangi ya upatanisho. Unajua, sayansi inajua ya kwamba kama ukichukua nyekundu na kuangalia kupitia nyekundu, kwa nyekundu, ni nyeupe. Angalia kupitia kwenye nyekundu, kwenye nyekundu, ni nyeupe. Yeye huangalia kupitia Damu nyekundu ya Bwana Yesu, na dhambi zetu nyekundu zinakuwa nyeupe kama theluji; nyekundu kupitia nyekundu.

Na huyo ndama aliuawa wakati wa jioni, na kusanyiko lote la Israeli.

Na pale paliwekwa milia saba kwa damu yake mlangoni ambapo kusanyiko lote lilipaswa kuingia; mfano wa zile Nyakati Saba za Kanisa, kwa Damu.

44 Na ndipo mwili wake ukachukuliwa na kuteketezwa kwa moto. Iliteketezwa kwa moto pamoja na kwato, pamoja na ngozi, pamoja na matumbo, pamoja na mavi. Kila kitu kiliteketezwa kwa moto, pamoja.

Na ilibidi achukuliwe na mtu msafi, na ilibidi kuwekwa mahali safi nje ya kusanyiko. Kwa hiyo, kama Israeli wangaliona tu mfano! Neno hili la Mungu halipaswi kubebwa na mikono michafu ya kutokuamini. Haina budi kuwa ni mtu msafi. Na kama yeye ni msafi, ilimbidi kupitia kwenye Chujio la Mungu.

Mtu safi, mikono safi, na ilibidi kuwekwa mahali safi; si mahali ambapo akina Yezebeli, na Rickies, na kila kitu wanashiriki; kula ushirika na kadhalika, wakati wanapokuwa wakizurura na wake, na waume, na kila namna ya uchafu; wakienda kwenye dansi na karamu, na kuwa na nywele zilizokatwa, na kaptura, na kila kitu kingine, na kujiita Wakristo. Linapaswa kuwekwa mahali safi, na kushughulikiwa kwa mikono safi.

Na ndipo Israeli walipotenda dhambi, na kutambua ya kwamba walikuwa wametenda kosa, basi walinyunyiziwa majivu ya ndama huyu, juu yao. Na hayo yalikuwa maji ya utengano, utakaso wa dhambi.

45 Angalia. Hili hapa! Na wakati Israeli, kabla hawajaingia katika ushirika katika ibada, iliwabidi kwanza kupitia kwenye maji ya utengano. "Kuhesabiwa haki kwa imani; huja kwa kusikia, kusikia Neno."

Ndipo wakaingia katika kusanyiko chini ya hiyo milia saba, ile damu, kuonyesha ya kwamba kitu fulani kilikufa na kutangulia mbele yao, kwa ajili ya dhambi zao. Walitengwa kwa kulisikia Neno, maji ya utengano, kisha wakaingia katika ushirika.

Mahali pekee ambapo Mungu alikutana na mwanadamu palikuwa nyuma ya utaratibu huo. Asingekutana naye mahali pengine popote. Ilimbidi kuja nyuma ya utaratibu huo. Mungu alikutana na Israeli mahali pamoja tu.

Na Mungu anakutana nawe leo mahali pamoja, na hapo ni katika Yesu Kristo; Naye ni Neno, maji ya utengano. Na Damu Yake ilimwagwa kwa ajili ya Nyakati zote Saba za Kanisa. Halafu basi, kwa Roho Mtakatifu, tunaingia katika ushirika huo, ambao hutolewa tu kwa Kanisa. Loo, jinsi Yeye alivyo mkuu!

46 Pia, sasa, tunataka kuangalia Waefeso 5:26, ilisema, "Ni kuoshwa kwa maji kwa Neno," maji ya utengano. Hufanya nini? Halafu, Chujio la Mungu ni Neno. Maji ya utengano, "kuoshwa kwa maji, ya utengano, kwa Neno," Chujio la Mungu.

Basi, huwezi kuingia katika Kristo kupitia chujio la kanisa. Huwezi kuja kwa chujio la kimadhehebu au chujio la kanuni za imani. Kuna Chujio moja tu, ambapo unaweza kuingia katika mahali pale patakatifu, hiyo ni kwa "kuoshwa kwa maji kwa Neno." Neno la Mungu ni Chujio la mtu mwenye busara.

47 Kanisa litakuhukumu hapa kama wewe ni mshiriki mzuri, ama la. Watakupa mazishi mazuri, na nusu mlingoti wa bendera wakati wa kufa kwako, watatuma mashada makubwa ya maua na—na kukufanyia kila kitu. Lakini inapofikia kwenye nafsi yako inayomkabili Mungu, haina budi kuwa na Uzima wa Milele. Na kama ni Uzima wa Milele, ni sehemu ya Neno. Na kwa kuwa neno langu mwenyewe haliwezi kukana …

Mkono wangu mwenyewe hauwezi kuukana mkono wangu. Macho yangu mwenyewe hayawezi kuukana mkono wangu, wala mguu wangu, wala kidole changu cha mguu, wala sehemu yoyote yangu. Haviwezi kuukana.

Na wala mwanamume ambaye ni sehemu ya Neno la Mungu, ama mwanamke, hawezi kukana sehemu

moja ya Neno la Mungu. Halafu, enyi wanawake, mnapofikiri mnaweza kukata nywele na kuja katika Uwepo wa Mungu, mmekosea. Mnaona jambo hilo? Umekosea; huwezi kuja kupitia kwenye Chujio la Mungu ambapo unaoshwa na maji ya Neno. Ndipo unaingia katika ushirika. Unafikiri uko hivyo, bali huwezi kuwa mpaka utakapopitia kwenye Neno, na kila sehemu ndogo, kila Neno dogo la Mungu. "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno." Haina budi kupitia kwenye huo mchujo, likipita moja kwa moja. Na hiyo inatoa ladha ya mtu mwenye haki, maana hiyo ndiyo anayoitafuta, akitafuta kitu fulani cha kumsafisha.

48 Neno, Neno la Mungu ni Chujio la mtu mwenye busara, na Hufanya ladha ya mtu mwenye haki. Tunajua hilo ni kweli; huchuja dhambi zote za kutokuamini. Hakuna kutokuamini tena unapopitia kwenye Chujio, kwa sababu ni ladha ya mwaminio wa kweli.

Mwamini wa kweli anataka kuwa sahihi, haidhuru. Hataki tu kusema, "Vema, mimi ni mmoja wa tabaka bora la kijamii. Mimi ni mfuasi wa kanisa, kanisa kubwa kuliko yote mjini." Sijali kama ni misheni fulani kule pembeni, kama ni mkutano wa nje, mahali fulani, mtu mwenye busara anajua ya kwamba hana budi kukutana na Mungu. Na haidhuru kanisa linasema nini, ama mtu mwingine ye yote asemaye, hana budi kuja kulingana na masharti ya Mungu. Na masharti ya Mungu ni Neno la Mungu.

"Vema," wao wanasema, "'Neno la Mungu.'"

Hakika, wote wanaamini ni Neno la Mungu, lakini unaweza kuchuja kupitia Hilo? Utamwachaje mwanamke aliyekata nywele zake apitie Pale? Utafanyaje jambo hilo? Utamwachaje mwanaume apitie Huko ambaye hatashikilia Fundisho hili? Mnaona?

Si ladha ya mtu mwenye busara. La. Mtu mwenye busara atafikiri, mtu mwenye busara atafikiri mara mbili kabla ya kurukia kitu kama hicho.

49 Angalia, Neno hilo haliwezi kujikana Lenyewe. Halafu limeridhika, ama ni shauku. Ni shauku ya nini? Ni kitu gani kilichokufanya na shauku hiyo, kwanza? Kwa sababu chini katika nafsi yako kulikuwako na mbegu iliyochaguliwa tangu zamani ambayo ilikuwa ni Uzima wa Milele, daima ikikaa mle ndani, daima ilikuwa mle ndani. "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu. Hakuna hata mmoja wao atakayepotea."

Ladha ya mtu mwenye busara, wakati mtu mwenye busara anapolisikia Neno la Mungu, "Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu, mgeni hawatamfuata," kwa maana ndani humo kuna Uzima, na Uzima unaungana na Uzima.

Dhambi huungana na dhambi, na dhambi ni ya unafiki sana hata inadhani ya kwamba imeokolewa wakati haijaokoka. Ni katika kilindi kabisa cha unafiki.

Washiriki wa kanisa wanataka chujio la kimadhehebu ili waweze kuwa na tamaa yao wenyewe na bado wahesabiwe kama watu "wa kidini". Unawasikia wakisema, "Loo, yeye ni wa kidini sana."

50 Huko Afrika, nilikuwa huko nje siku moja, nao walikuwa wakizungumza juu ya hizi, baadhi ya watoto walikuwa wakizungumza juu ya nyimbo hizi za rumba ambazo Elvis Presley na hao wengine walikuwa wakiimba, Pat Boone na kadhalika, Ricky Nelson na hao wengine wote. Nikasema, "Hao ni kundi la wasaliti."

Msichana fulani mdogo alisema, "Mbona, yeye ni wa kidini sana."

Nikasema, "Vivyo hivyo na Yuda." Nikasema, "Yuda alipata tu vipande thelathini vya fedha; Elvis Presley alipata dola milioni kadhaa." Mnaona? "Wote wawili waliuza haki zao za mzaliwa wa kwanza." Mnaona? Nikasema, "Hao si- … deni kubwa sana taifa lililo nalo." Bado, ni udanganyifu tu kama chujio la sigara, madhehebu haya yanawaruhusu hao washiriki kuingia. Hata hawakupaswa kuwa … Kunapaswa kuwe na sheria kwamba wasingeweza kuimba nyimbo za dini. Ni kinyume cha … inapaswa kuwa ni kinyume cha sheria kwao kufanya hivyo.

Lakini jambo hilo lote limekuwa lundo moja kubwa sana la unafiki, na hapo ndipo wanapokaa leo. Chujio la kweli kwa ajili ya nafsi, linasema, "Ukiipenda dunia au mambo yaliyomo katika dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako."

51 Unaona, huwezi—huwezi kusema rumba ni la ulimwengu … ama ni la Mungu. Rumba ni ya dunia. Yoyote ya hizo dansi na kuchujwa … mambo machafu mabaya, hasa, ni ya dunia. Yote ni ya dunia.

Huwezi kusema ya kwamba nywele zilizokatwa kwa mwanamke ni za Mungu. Biblia inasema sivyo, kwa hiyo ni uchafu wa dunia. Na kama ukipenda chembe moja ya ulimwengu, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako. Mnaona?

Ni kitu gani hicho? Vema, ni kitu gani kinachoivuta? Ni kitu fulani huko ndani kinachovuta. Nafsi inachota rasilimali yako kupitia nje, kushuka kupitia kwa roho, kuingia kwenye nafsi. Na kama nafsi inaipenda dunia, imekufa. Sijali jinsi ilivyotiwa mafuta, iko hapa nje, na jinsi ilivyo wa haki hapa; chini hapa imekufa. "Kwa maana yeye aipendaye dunia ama mambo ya dunia, kumpenda Mungu hata hakumo

ndani yake," haidhuru ni wa kidini iliyoje.

Chujio la kweli, kwa njia hiyo, lita—litaweka mambo hayo yote nje na halitaleta kitu ila ukweli wa Mungu, Neno, katika nafsi halisi na ya kweli.

52 Wao ni kama Esau, wako sawa kwa nje. Esau alikuwa wa kidini kwa nje. Na inapofikia kwenye dini, ilionekana alikuwa wa kidini zaidi kuliko Yakobo alivyokuwa. Alionekana kuwa mtu bora kuliko Yakobo alivyokuwa, bali ndani yake, jinsi alivyokuwa. Alikuwa wa kidini kwa nje, bali mawazo yake hayakuchujwa. Yeye hakuwazia sahihi kuhusu haki ya mzaliwa wa kwanza. Yeye—yeye hakufikiri ya kwamba Mungu, haki ya mzaliwa wa kwanza ilimaanisha kadiri Mungu alivyosema ilimaanisha. Huyo hapo, kasema, "Nina njaa, inaleta tofauti gani kuhusu ile haki ya zamani ya mzaliwa wa kwanza? Unaweza kuipata ukitaka." Loo, jamani! Mnaona?

"Ninaenda kanisani; Mimi ni mwema tu kama mlivyo ninyi. Madhehebu yangu ni kama tu … Mbona, ni moja ya yaliyo makuu sana ulimwenguni. Mama yangu alikuwa mfuasi wake. Baba yangu alikuwa mfuasi wake. Yote haya, yale, na mengineyo. Mchungaji wangu alikuwa na elimu; ana kitu fulani na fulani." Hilo linamweka mbali sana na Mungu. Hilo si chujio la mtu mwenye busara.

Kama lingekuwa, Petro angewezaje kuwa vile alivyokuwa, wakati asingeweza kuandika jina lake mwenyewe? Lakini yeye alibeba Chujio la mtu mwenye busara. Angalia. Loo, jamani!

53 Esau alifikiri ya kwamba haki hiyo ya mzaliwa wa kwanza haikumaanisha kile Mungu alichosema ilimaanisha. Hiyo ndiyo iliyokuwa tofauti kati ya Uzima na mauti. Na kwa hiyo, kama vile Hawa na kama Yuda, waliuza haki zao za mzaliwa wa kwanza kwa kuridhika na ladha ya maarifa ya ustaarabu. Hivyo ndivyo hasa Hawa alivyouza haki zake za mzaliwa wa kwanza. Aliiuza kwa ladha kidogo ya sayansi, ladha kidogo ya maarifa ya kilimwengu, kanisa bora zaidi, tabaka bora zaidi la watu, leo itaitwa. Mnaona?

Naye Yuda aliuza haki yake ya mzaliwa wa kwanza kwa vipande thelathini vya fedha, na kupata dola chache za ziada. "Kusanyiko langu linaweza kunilipa vizuri zaidi hapa, nami nitahubiri hapa tu." Mnaona? "Kwa hiyo, kama nikifanyika mhubiri, vema …"

54 Walisema, "Ndugu Branham, tunaamini Ujumbe huo ni Kweli, bali hatuwezi kuukubali. Kama tungefanya hivyo, mbona, tungehubiri wapi?" A -ha! Ulimwengu, ndugu, hiyo ni parokia. Hakika. "Vema, hakuna ndugu yeyote ambaye angeniunga mkono." Mimi—mimi simtafuti ndugu yeyote wa kuniunga mkono. Ninamtazamia Yesu Kristo kuniunga mkono, kwa sababu Yeye alisimama Nalo. Yeye Ndiye aliyelisema.

Na wakati haki ya mzaliwa wa kwanza, ile Damu, ilipochujwa na Neno; na dhambi zote, na ulimwengu, na kanisa, na madhehebu, na dini, vimeachwa nje. Elimu, ustaarabu, kanisa, madhehebu, mfumo, dhambi za kila namna huachwa nje wakati mtu mwenye busara anapochuja Chujio la mtu mwenye busara, katika kadirio la Mungu.

Hakuna kitu kilichosalia ndani yake wakati mtu anapovuta yake—maisha yake kupitia Chujio la Mungu; angalia, hapa maisha yako yalikuwa yamechanganyikiwa na dhambi, kwa sababu "ulizaliwa katika dhambi, ukaumbika katika uovu, ukaja ulimwenguni ukisema uongo."

Nitasema jambo fulani, kama vile Ndugu McCullough alivyokuwa akisema. Nisikilizeni.

55 Ulipokuja katika ulimwengu huu, ulizaliwa katika dhambi. Hata hukuja na nafasi ya kupigana. Wewe "ulizaliwa katika dhambi, ukaumbika katika uovu, ukaja ulimwenguni ukisema uongo," ndani ya roho yako mwenyewe, tamaa ya dhambi, mpenda dhambi kwa sababu ulizaliwa katika dhambi. Hukuwa na nafasi. Lakini chini ndani yako, mahali fulani, hapa unakuja, kulikuwa na kitu fulani mle ndani kilichoanza kuvuta. Kama ulijua, ilikuwa ni kitu fulani kilichokwambia kulikuwa na Mungu mahali fulani; nawe unasoma Neno Lake. Ndipo ukachukua kanisa, ukachukua mawazo yao ulipoambiwa vema, basi hukutumia Chujio la mtu mwenye busara. Bali unapotumia Chujio la Mungu, ambalo ni Chujio la mtu mwenye busara, kwa sababu, "Machujio mingine yote yatapita, bali Langu halitapita." Na unapochukua Chujio la Mungu na kuyavuta maisha yako, tamaa zako; kama ukivuta tamaa zako kupitia Chujio la Mungu, Chujio la mtu mwenye busara, hakuna kitu kilichosalia ila Roho Mtakatifu.

Sasa, kama unataka ushahidi wa Roho Mtakatifu, huo hapo. Wakati hiyo nafsi yako itakapolingana na Neno la Mungu, katika kila hali, inaonyesha umevuta maisha yako kupitia Chujio la mtu mwenye busara, Chujio la Mungu.

56 Angalia, hilo ni Chujio la Mungu? Yeye alisema, "Tulioshwa kwa maji ya Neno."

Na wakati Mungu alipowapa Adamu na Hawa Kichujio, katika bustani ya Edeni, Yeye alisema, "Usivute cho chote cha haya mle ndani." Lakini Shetani alitoboa tundu ndani Yake, akasema, "Loo, ni kidogo, haitadhuru." Tone moja tu, kupitia, yote ndiyo iliyohitajika kuweka mauti katika jamii ya binadamu.

Hivyo tu ndivyo inavyohitajika, ladha moja tu ya nikotini, kisha wameondoka.

Hakuna kitu kilichosalia ila Roho Mtakatifu.

Na halafu hiyo inaonyesha ya kwamba ndani yako kulikuwa na ile mbegu iliyochaguliwa tangu zamani ndani yako, hiyo inakufanya uwe na njaa ya Mungu. "Wote alionipa Baba, amenipa mimi kuwakomboa; walikufa pamoja Nami pale Kalvari; walifufuka pamoja nami katika ufufuo; wote ambao amenipa Mimi, watakuja Kwangu. Yatawekwa katika Mwili, ambapo mguu, mkono, pua, kinywa, cho chote kile; watawekwa mle. Nao watanijia katika majira yao." Loo, jamani!

57 Huko kuna kule kuchujwa halisi kwa dhambi zote za ulimwengu, na kuipenda dunia kumekufa, na nafsi hii inavuta kitu kimoja tu. Hii hapa, usininii … Kumbuka! Usisahau jambo hilo. Ninyi nyote mlio huko nje kwenye simu, wekeni jambo hili moyoni mwenu. Wakati mtu mwenye busara anapoanza kuwazia ni nani atakayesimama mbele zake, na Neno la Mungu ni nini; wakati anapoanza kuwazia, ndipo anapochukua jambo Hilo, hakuna kitu kinachoweza kulifikia ila Roho Mtakatifu.

Ni kitu gani? Ni chembechembe hai, mbegu Neno tangu mwanzo, kwamba ulikuwa katkai Mungu hapo mwanzo, ukisimama hapa ukivuta Uhai wa mbegu. Ile mbegu iko moyoni mwako, kwa kujulikana tangu awali. Haleluya! Ile mbegu tayari imo mle ndani, kwa kujua tangu zamani kwa Mungu, imechaguliwa tangu zamani. Na wakati inapovuta, haiwezi kuvuta kitu kingine ila Neno.

Halafu basi ni ladha ya mtu mwenye busara, mtu mwenye haki, mtu mtakatifu anayeiona Biblia, ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana na hata milele. Ni kitu gani kinachokuja mahali hapo chini? Hilo Neno, lililoko moyoni. "Nimelificha Neno Lako moyoni mwangu, nisije nikakutenda dhambi."

Ni kitu gani, wakati kinapopitia katika Neno? Kuna jambo moja tu litakalopita katika Neno; huyo ni Roho Mtakatifu. Hicho ndicho kitu pekee kinachoweza kupita katika Neno, ni Roho Mtakatifu. Na Chujio la mtu mwenye busara humpa mtu mtakatifu ladha.

58 Halafu, ameonja mambo ya Mbinguni; yeye ana Neno la Mungu moyoni mwake. Yeye huliona likidhihirishwa mbele zake, na nafsi yake yote imefungwa ndani Yake, na ulimwengu na vitu vyote vinavyomzunguka vimekufa.

Chujio la mtu mwenye busara, la dini; nami ninawazia kuichuja dini sasa. Wakati Chujio la mtu mwenye busara linapotoa ladha ya mtu mtakatifu, unaona, linaridhisha ladha yake. Anaona ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Hilo hapo. Tunamwona moja kwa moja mbele zetu, akifanya mambo yale yale aliyofanya; linaridhisha ladha ya mtu mtakatifu, kufikiria kwake.

Yeye anajua basi ya kwamba amepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Naye anapenda, na—na—na inapenda ulimwengu … kuthibitishwa, na anataka Neno lihakikishwe na kuthibitishwa. Katika kila wakati yeye huungojea, kwa kuwa yeye ni mtu mtakatifu na ana shauku ya kumwona Mungu. Wengine wanataka tu kujiunga na kanisa. Mtu huyu anataka kumwona Mungu. Yeye hamwoni katika kundi la kanuni za imani. Yeye hamwoni Yeye katika vyombo vikubwa vya zumari, ama makanisa makubwa ya majimbo, na misalaba mirefu, ama wanachuoni waliogharishwa wakiwa na kola zao zigeuzwa. Yeye hamwoni katika theolojia na katika mwanatheolojia. Yeye humwona katika thibitisho la Neno Lake.

> Nilimwona Yeye katika mioto yake ya ulinzi.
> Macho yangu yameona utukufu wa kuja kwa Bwana;
> Yeye anakanyaga panapo hifadhiwa zabibu za ghadhabu;
> Yeye ameuachilia umeme wa kuangamiza na upanga Wake mwepesi wa kutisha;
> Ukweli Wake unaendelea kusonga mbele. (Itakuwa, hata mwisho. Naam, bwana.)

59 Mnaona ninalomaanisha? Chujio, mwanadamu … Ama, Chujio la mtu mwenye busara; mtu anayetaka kusimama katika Uwepo wa Mungu. Chujio la Mungu lilikuwa nini? Neno Lake. "Siku utakayokula, siku hiyo utakufa." Sijali kinachotendeka hapa nje; usipite Neno hilo. "Kuoshwa kwa maji ya Neno," Chujio la mtu mwenye busara. Si dhehebu, si kanuni ya imani, si kanisa, si kanisa kuu; bali ni Chujio la mtu mwenye busara, kwa maana utahukumiwa kwa Neno. Mtu mwenye busara atafikiri hivyo. Mtu mpumbavu, ama ladha ya ulimwengu, atachukua tu chochote, kibadala. Kwa nini ubadilishe wakati kuna Yule halisi?

60 Wazia, hebu wazia jambo hilo kwa dakika moja. Mwanamke anayenena kwa lugha, akiwa na nywele zilizokatwa na rangi za mdomo, na halafu kanisa lingali linashikilia jambo hilo, ya kwamba huo ndio uthibitisho wa Roho Mtakatifu.

Ama mhubiri kutoka seminari ama shule fulani ya Biblia, akitumia ubatizo wa utatu, ama kupatana na Neno, kwa kanuni fulani za imani ama dhehebu. Je! Hilo ni Chujio la mtu mwenye busara? Si jinsi ninavyoona jambo hilo, ndugu. Ni mtu mpumbavu anayepitia hayo. Hiyo ni kweli. Ungeweza kuwazia jambo hilo? Badala ya kutumia Neno la Mungu kama Chujio kwa nafsi yake; akiruhusu kanuni hiyo ya kale ya imani na madhehebu yajikusanye juu yake namna hiyo, badala ya kuchukua Neno la Mungu kama Chujio. Na ndipo yeye amechafuliwa kabisa, na kuwaacha waingize ndani yake mafundisho ya mwanadamu, wakifanya mambo, "karibu kuwadanganya walio Wateule," na kupuuza Neno.

Wakati, angeweza kuvuta kwenye nafsi yake mwenyewe, kama kuna cho chote mle ndani cha

kuvuta. Lakini kama mbegu hiyo iliyochaguliwa tangu awali … Usikose jambo hili. Kama hiyo mbegu iliyochaguliwa tangu awali haimo mle ndani, haitavuta kupitia Mle, kwa sababu itavuta kwa ajili ya tamaa yake.

61 Kama mtu anayevuta sigara anataka ladha ya mtu anayevuta sigara, na kama alikuwa ameshika fimbo … Ninasema, "Nyonya kidole chako," naye akasimama pale akinyonya kidole chake. [Ndugu Branham ananyonya kidole chake, kuonyesha — Mh.]

Mbona, angesema, "Huo ni upumbavu." Kwa nini? Ladha yake ni kwa ajili ya nikotini. Kwa hiyo, yeye si mtu mwenye busara. Mnaona? Lakini unasema, "Vema, sijui, sitaonja chochote. Ninataka kuonja ninii … Ninataka kuonja tumbaku. Sionji kitu."

Mpe kibanio cha nguo na mwache anyonye hicho. Mnaona? Hakika, hebu anyonye hicho. Yeye anasema, "Sionji kitu." Unanyonya kwa ajili gani, basi? Una shauku ya kuonja nikotini.

Na wakati unaponyonya kanuni ya imani ya kanisa, na bado ninyi wanawake mnakuwa na nywele zilizokatwa, nyuso zilizopakwa rangi, na mmevaa kizinifu; na wewe mwanaume unawatazama, na mambo haya mengine yote, na uendelee jinsi unavyofanya. Ni kitu gani? Kuna nini mle ndani? Ulimwengu ungali mle ndani, nanyi mna ladha. Unaivuta kwa ladha.

62 "Ninaenda kwenye kanisa hili; kamwe hawataji kitu hicho. Hawasemi lo lote kuhusu jambo hili, wala kuhusu jambo hilo. Hakuna hata moja ya mambo haya yanayoibuliwa. Mhubiri wetu ana mawazo mpana zaidi kuliko hayo. Hatusemi mambo kama hayo." Ni kitu gani? Una ladha ya ulimwengu unaounyonya. Sawa!

Lakini mwanamke mwenye busara hatachukua kitu kama hicho. Yeye anajua hana budi kuwa mtakatifu. Na kitu pekee unachoweza kuchota kupitia Neno la Mungu ni Roho, Nguvu za kuhuisha kulifanya Neno Lenyewe, ambalo limo ndani yako, liishi lipate kumdhihirisha Yesu Kristo katika wakati unaoishi. Haleluya! Ndugu, kama hiyo si Kweli, sijui Kweli ni nini. Nimerukwa na akili kama hiyo si Kweli.

Ni Neno Lenyewe moyoni mwako, lililochaguliwa tangu awali pale, ambalo linavuta. Na linautema ulimwengu huo; haliutaki. Lakini linapofikia hapa katika Neno, linaanza kuvuta. Na wakati linapopitia kwenye Neno, haliwezi kuwa kitu kingine ila Roho Mtakatifu kulihuisha Neno hilo.

63 Ndipo Chujio la mtumwenye busara wa kidini, ni Neno, nalo linaridhisha ladha hiyo takatifu iliyo moyoni mwake; chujio la mtu mwenye busara, ladha ya mtu mtakatifu. Loo, jamani, tumo kwenye nini!

Badala ya kutumia Chujio la Mungu kwa ajili ya nafsi yake, yeye anamwacha Shetani amdanganye kwa madhehebu fulani ama kanuni ya imani, kama tu vile makampuni ya tumbaku yanavyowadanganya ninyi watu mnaovuta sigara. Mnapata tu washiriki wengi zaidi, na hivyo tu.

Loo, hebu nifunge kwa dakika chache, nikisema jambo hili.

64 Laodikia kipofu! Jinsi tunavyoweza kuwa vipofu! Laodikia kipofu, akiwaongoza vipofu wa wakati huu, chini ya uongo, chini ya kanuni za imani za uongo, chini ya mafundisho ya sharti ambayo ni ya uongo, chini ya madhehebu ambayo ni ya uongo, chini ya vitabu vya kanuni za imani ambavyo ni uongo. Loo, ewe Laodikia kipofu, ukiwaongoza vipofu, nyote mnaelekea shimoni!

Badilisha chujio lako usiku wa leo, mhubiri. Usiingize hiyo nikotini ya kimadhehebu katika mfumo wako, wa mafundisho ya sharti na kanuni za imani, ambayo Yesu alisema, "Ye yote atakayeongeza neno moja Kwake, ama kuondoa Neno moja Kwake." Unapoliambia kusanyiko lako ni sawa kwa hao wanawake kufanya hivyo, na hao wanaume kufanya hivyo, na mambo haya yote, yale na mengineyo; mradi tu wanadumu waaminifu kwa hili na kufanya lile, na kushika kanuni hizi za imani na kadhalika, hivi huoni haya?

"Mafarisayo vipofu," Yesu alisema.

65 Na wakati Yesu alipopaza sauti, "Mafarisayo vipofu," Roho Mtakatifu katika moyo wangu mwenyewe usiku wa leo analia, "Laodikia kipofu! Ni mara ngapi Mungu angekupa ufufuo! Lakini sasa wakati wako umewadia; umechelewa sana sasa. Ulichekaje na kuwadhihaki watu ambao Mungu aliwatuma kwako! Lakini sasa wakati wako umewadia. Loo, Marekani, Marekani, jinsi ambavyo Mungu angaliwafunika kama vile kuku—kuku anavyoatamia vifaranga vyake, lakini hamngekubali." Sasa Sauti hii inaenda kutoka pwani hadi pwani, kutoka kaskazini hadi kusini, na mashariki hadi magharibi. Jinsi ambavyo Mungu angaliwafunika, lakini hamngekubali! Sasa wakati wako umewadia.

Mataifa yanavunjika. Ulimwengu unaporomoka. Kipande chake cha maili elfu moja na mia tano, upana wa maili tatu au mia nne, kitazama, mia … ama labda maili arobaini chini kwenye ufa huo mkubwa huko ng'ambo, moja ya siku hizi, na mawimbi yataruka juu hadi kwenye jimbo la Kentucky. . Na kitakapozama hivyo, kitautikisa ulimwengu kwa nguvu sana hata kila kitu kilicho juu yake kitatikisika.

Loo, nifiche katika Mwamba wenye imara! Mungu, nijalie, nijalie. Nipulizie, Bwana. Roho wa Mungu aliye hai, nipulizie. Hebu nichukue Chujio la Mungu na niishi chini ya Hilo, Bwana. Hebu nipumue hewa safi ya Roho Mtakatifu katika mapafu yangu, katika nafsi yangu kila siku, nisije nikakutenda dhambi, Ee Bwana. Nipulizie, Roho Mtakatifu, nipulizie! Mimi …

66 Hebu nipande Neno la Mungu moyoni mwangu, na kusudi la hapo kwamba sitageukia mkono wa kuume wala wa kushoto, mbali na Hilo, bali nitaishi kwa uaminifu Kwake siku zote za maisha yangu. Ee Baba Mungu, basi nitumie Roho Mtakatifu wa Uzima, juu yangu, kuyahuisha hayo Maneno kwangu, ili nipate kumdhihirisha Yesu Kristo mbele ya wale walio mbele yangu, kulitazamia litukie. Hayo ndiyo maombi yangu.

Loo, jamani! Angalia jinsi wanavyofanya leo katika makanisa hayo. Kuwanyonya watu kupitia kwenye vishungi hivyo vya kimadhehebu, katika baraza la ekumeni. Kwa nini? Kwa nini? Kwa kuwa inawapa tamaa ya mioyo yao, madhehebu. Wana ladha ya madhehebu. Watafanya hilo.

Kila wakati Mungu alipowatumia uamsho, na, wao, walifanya nini? Wanayaundia madhehebu. Hiyo ni kweli? Kwa hiyo wana chujio la aina yao, kwa sababu wana ladha nzuri. Na sasa Mungu atawapa tamaa yao ya ladha yao. Yeye atawapa … Wanawanyonya moja kwa moja kwenye baraza la ekumeni, kisha wanapata ladha yao ya kimadhehebu basi. Wao wanayo inakuja.

67 Loo, enyi kanisa la Laodikia, msidanganyike katika wakati huu, kwa udanganyifu wao. Loo, Pentekoste, ninyi mlioingia Laodikia, ninyi mlio sehemu ya Laodikia, kanisa lililokufa; kupitia Methodisti, Baptisti, na Presbiteri, utaratibu tu wa kimila. Lakini ninyi Wapentekoste ambao bado mara moja moja mngaliweza kusema "amina"; ambao mnaweza kupiga muziki mwingi jukwaani, na kuwa na wanawake waliokata nywele zao wakicheza kila mahali, na bado mnaamini katika uponyaji wa Kiungu; ni mara ngapi Mungu angewakuchukua, bali mlichukua chujio lingine, chujio la kimadhehebu. Ni mara ngapi Mungu angewachukua!

Jinsi lilivyokuwa la udanganyifu! Mathayo 24:24, Yesu alisema ya kwamba … "Ingewapoteza walio Wateule kama yamkini." Jinsi mlivyo karibu, kama tu vile Hawa, ukiacha tu kitu kimoja ama viwili vidogo ambavyo msingepokea, kwa sababu umeunda madhehebu na huwezi kulipokea. Hilo tu ndilo linalohitajika. Afadhali tu uchukue jambo lote, "Kwa kuwa kukosea katika lililo dogo, ana hatia ya jambo lote." Loo!

68 Pentekoste, Pentekoste, pitisha mawazo yako kupitia Chujio la Mungu, si ndoto zako za kimadhehebu, nawe utatoka na ladha ya mtu mtakatifu, ubatizo wa kweli wa Roho Mtakatifu.

Ungeweza kuwazia mwanamume akimwacha mke wake akate nywele zake, kuvaa kaptura, ama kuvaa suruali, na kusema anapitia kwenye Chujio la mtu mwenye busara? Ungeweza kuwazia mtu akifanya jambo kama hilo?

Waweza kuwazia mhubiri amesimama mimbarani, kwa sababu analipwa vizuri kwa kusanyiko linalompigapiga mgongoni, anamwita, "Daktari, Ndugu, Kasisi," na kumpeleka kwenye karamu za kila namna ambako wanaume na wanawake wanaogelea pamoja, na kila kitu kingine, kwenye fukwe; ungeweza kuwazia mtu akidai ya kwamba anakuja kupitia Chujio la mtu mwenye busara?

Na baadhi ya hao wanawake kwenye jukwaa, wakiwa na nguo zao juu ya magoti yao, na imeshonwa ikiwa imebanwa sana na inaonyesha kila umbo, kila hatua wanayopiga, na nguo zao za ndani zikionekana ndani ya nguo zao; mbaya tu kama kuvaa kaptura, bikini, ama cho chote kile. Ninyi Wapentekoste, vipofu, wahubiri wa Laodikia, Mungu atawavumilia mpaka lini, sijui. Kuwa … Mungu na awe na rehema kwa—kwa macho yenu vipofu. Yeye ana dawa ya macho usiku wa leo, kuyafungua macho yenu, mpate kuona.

69 Kama nilivyosema asubuhi ya leo, tuko katika wakati wa kuona, kileleni. Hakuna nguvu zingine za kiakili juu ya hiyo, ambapo unaweza kwenda juu zaidi, kujua. Wewe, kutoka pua yako, unaweza kunusa; kutoka midomoni mwako, unaweza kunena; kutoka mikononi mwako, unaweza kuhisi na kufikia; na miguu yako, na kadhalika; bali huwezi kwenda mbali zaidi ya macho yako.

Malaki 4 imekuja; kuona! "Na itakuwepo Nuru wakati wa jioni." Loo, tembea katika Nuru!

> Tutatembea Nuruni, Nuru nzuri,
> Hilo huja ambapo matone ya umande wa rehema ni angavu;
> Niangazie kunizunguka mchana na usiku,
> Yesu, Neno, Nuru ya ulimwengu.

Naam, bwana. Pitia Hilo, loo, ndugu, nawe utatoka na ladha ya mtu mtakatifu, pamoja na Roho Mtakatifu.

70 Loo, mwanamke, acha tu mawazo yako ya kisasa kuhusu mavazi. Pitisha mawazo yako ya kisasa, kabla hujaenda mtaani mbele ya mwanaume; enyi wanawake vijana, enyi wanawake wazee, kabla hamjaenda mtaani huku nguo zenu zimekubana sana, zimesukumwa nje huko nyuma na mbele. Mimi si

mkosoaji. Mimi ni ndugu yenu. Ninasimama kati ya walio hai na waliokufa, na kutambua yale ninayosema. Kabla hujaingia, na kujua ya kwamba mwili wako ni chombo kitakatifu, ama jengo takatifu ambalo Mungu amekupa; kabla hujaingia barabarani, umevaa namna hiyo, pitisha akili yako kwenye Chujio la mwanamke mwenye busara. Na hebu kumbuka, ya kwamba, "Kila mtu anayekutazama kukutamani, tayari umekwisha kuzini naye." Kumbuka jambo hilo, dada.

Na, ndugu, kabla hujageuza kichwa chako kumtazama, kwa mtazamo huo wa pili, pitishaa akili yako kwenye Chujio la mtu mwenye busara. Utatoka na ladha ya mtu mtakatifu, unaona, ya kufanya yaliyo mema.

71 Angalia, kama ukipitisha akili yako katika Chujio la mwanamke mwenye busara, utatoka na mavazi ya mwanamke mtakatifu. Hiyo ni kweli. Utatoka, ndugu, ukiwa na sura ya mtu mtakatifu. Sasa, hilo ni jambo moja tu.

Kila kitu unachofanya, kipitishe katika Chujio la Neno la Mungu, uone kama ni kweli ama si kweli.

Utatoka na mavazi ya mwanamke mtakatifu, mwenye nywele ndefu, amevalia kwa heshima; roho tulivu, nyenyekevu; siyo ya hasira na ugomvi wa kelele na kupigana na kufanya yasiyofaa. "Roho ya utulivu, upole, ambayo ni hazina kuu kutoka kwa Mungu." Biblia ilisema hivyo.

Sasa nataka kuwaulizeni jambo fulani, huko nje katika nchi. Tutafunga katika dakika chache.

72 Sasa hebu sisi sote, usiku wa leo, tuchunguze tamaa zetu, na ndipo unaweza kuona ni aina gani ya chujio ambalo umekuwa ukipitia. Hebu na tuchunguze, kila mmoja wetu, hapa na kote nchini. Chunguza tamaa zako, kile unachotaka hasa maishani. Angalia kile unachopigania. Angalia umekuja hapa kwa sababu gani. Angalia ni kwa nini unaenda kanisani. Kinachokufanya … Ni vizuri kwenda kanisani, lakini usiende tu kanisani; hilo halitakuokoa. Mnaona? Angalia tu dakika chache, useme, "Je! Kusudi langu … Nina—ninavutia katika chujio la namna gani, hata hivyo?"

Na kama hutaweza kukabiliana na Neno la Mungu, na nafsi yako haifanyi hivyo, basi kuna kasoro; kwa kuwa inaonyesha ladha yako, ya kwamba uhai … ni uhai wa namna gani ulio ndani yako. Kama ni mtakatifu, mwenye busara, mwenye heshima, utatokea namna hiyo. Kama sivyo, una ladha nyingine ndani yako unayovutia. Hiyo ni kweli kabisa.

Na kama ladha ni Neno la Mungu na mapenzi ya Mungu, basi unajua kilicho ndani yako, kile kinachovuta ladha. Inaonyesha wewe ni sehemu ya hilo Neno. Hilo Neno limo ndani yako, likivuta toka kwenye Neno.

73 Linavuta nini? Linavuta kupitia Neno, kwa sababu wewe ni sehemu ya Mwili wa Kristo wa wakati huu. Na kama Neno hilo liko ndani yako, linaweza tu kuvuta kupitia Neno, Roho anayehuisha Neno hilo lililo ndani yako. Ni Neno pekee tu halitaishi. Hiyo ndiyo sababu, "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu; na kama nikiinuliwa juu, nitawavuta watu wote Kwangu." Mnaona? Mnaona, "Baba," sehemu ya Mwili wa Kristo ulio ulimwenguni, uliochaguliwa tangu zamani, unawekwa moyoni.

Mtu yeyote ambaye ni Mkristo halisi, aliyezaliwa mara ya pili leo, anajua, tangu alipokuwa mtoto mdogo, ama msichana mdogo, yeyote yule, ya kwamba kulikuwa na kitu fulani ndani yako kilichomwonea Mungu njaa. Nawe ulijaribu kujiunga na makanisa na cho chote kile; isingefaa kitu. Ilikuwa ni kitu gani? Ilikuwa ni hilo Neno. Ulikuwa ukitafuta Chujio. Na siku moja iliangaza mbele yako; ulimwona Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Hilo liliridhisha ladha. Mnaona?

Maana, uhai ulikuwa ndani yako, ukivuta. Unaona, uhai ulio ndani yako unavutwa. Una—unaelezea ni shauku gani uliyo nayo hapa. Unavuta. Huwezi kuvuta kupitia hili, na lile, na lingine. Huna budi kupata Chujio hilo sahihi, maana wewe ni mtu mwenye busara. Mnaona?

Kama wewe ni mtu mwenye busara, umechaguliwa tangu awali, ama umechujwa kabla … kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

74 Na kama mhudumu wa kimadhehebu akisikia hili, natumaini ya kwamba atachukua Chujio la mtu mwenye busara, kama yeye ni mhudumu wa madhehebu. Ndipo yeye atatupilia mbali hiyo pakti ya kimadhehebu ambayo haina budi kuangamia, maana ni neno la mwanadamu; na akubali Neno la Mungu lililochujwa ambalo kamwe haliwezi kushindwa wala kupita, na litafaa ladha ya mtu mtakatifu. Na, kama vile Yakobo, ataacha ulimwengu wote na tamaa za kidhehebu ama sifa, zilizomo ulimwenguni, ambapo unaweza kuwa askofu, kadinali, ama unaweza kuwa mzee wa jimbo, ama mchungaji wa kanisa fulani kuu. Utaacha kila kitu kilichopo. Si kama Esau, kuwa sehemu ya ulimwengu; lakini kama Yakobo, utatoa kila kitu ulicho nacho kupata haki ya mzaliwa wa kwanza, Chujio la mtu mwenye busara; Maana litakupa ladha ya mtu mtakatifu. Nayo itaridhisha. Na itaridhisha, na itatakasa kwa ladha ya Milele ya wema mtakatifu wa Mungu.

75 Kumbukeni, Shetani alitoboa tundu la kwanza katika nia ya Hawa, ama kufikiri kwake, kuruhusu ladha

ya hekima yake na maarifa yaingie.

Sasa wazia jambo hili. Ninafunga. Shetani alitoboa tundu la kwanza moja kwa moja, maana yote aliyoweza kuvuta ilikuwa ni Neno. Huyo alikuwa ni Roho kupitia Neno la Mungu, maana alisema, "Mradi tu unapumua kupitia Chujio hili, hutakufa kamwe; bali ukivuta pumzi kutoka kwenye hii hapa, utakufa." Mnaona?

Naye Shetani akasema, "Lakini hujui kitu hapa. Lakini hebu onja hii kidogo hapa, ndipo utajua; utakuwa kama Mungu. Mnaona, Yeye anajua mema na mabaya; wewe hujui. Na kama utaonja tu ladha ya hii kidogo." Naye akamwachilia atoboe tundu ndani yake, shimo moja dogo tu.

Sasa mnaona ni kwa nini ninasema … Unasema, "Kwa nini usiwafundishe wanawake, na kadhalika, namna ya kupokea karama na vitu kama hivyo?"

Nikasema, "Unawezaje kuwafundisha aljebra wakati hawajapata kujifunza ABC zao?"

Tundu moja dogo ndilo lililohitaji. Yeye alichukua hekima ya ulimwengu, na, wakati lilipotukia, lilileka mauti kwa jamaa yote, kutaka kuonja hekima.

76 Sasa angalia chujio, na hakika lilionyesha shauku yake. Shauku yake ilikuwa ni kwa ajili ya ulimwengu; hicho ndicho alicho nacho. Hivyo ndivyo ilivyo leo. Wanaupenda ulimwengu na mambo ya ulimwengu, kwa mfano wa utauwa, bali wakikana Nguvu zake. Mnaona, Shetani atawaruhusu kunena kwa lugha; atawaacha wapaze sauti; atawaacha wafanye ibada za Kiungu za uponyaji; atawaacha wafanye mambo ya namna hii yote.

Yeye alisema, "Wengi watakuja Kwangu katika siku hiyo, na, 'Bwana, si niliwatoa pepo, sikufanya mambo mengi, nikafanya jambo hili?'" Yeye atasema, "Hata sikukujua, wewe mtenda maovu." Wakati Neno lilipowekwa moja kwa moja mbele zako na ungali ukanyonya ile chujio la kale la ulimwengu, mnaona, inaonyesha ladha iliyokuwa moyoni.

77 Njiwa hawezi kula mzoga uliooza. Hawawezi kula. Hawana nyongo yo yote. Kunguru anaweza kula mbegu kama hua na anaweza kula nyama iliyooza kama kunguru, mnaona, kwa sababu yeye ni mnafiki. Lakini hua hajajengwa kama ndege mwingine yeyote, na hiyo ndiyo sababu Mungu alijiwakilisha Mwenyewe kama Hua akishuka kutoka Mbinguni. Mnaona? Hawezi—hawezi kuvumilia uvundo wa nyama iliyooza. Yeye siyo tai; sababu, hana nyongo yo yote. Asingeweza kumeng'enya. Ingemwua, kama angekula.

Na hua kamwe haimbidi kuoga. Mwili wa hua hutoa mafuta kutoka ndani, ambayo humweka safi. Ni uzima uliyo katika hua; unazalisha ndani yake mafuta ambayo yanaweka manyoya safi. Na vivyo hivyo na Mkristo; kuna Uzima ndani yao unaowaweka safi. Umechujwa.

Loo, angalia! Sasa mwangalie yeye … kwenye chujio, na hakika unaweza kuona ladha yake, ya yale wanayofanya leo.

78 Angalia kanisa hili la kisasa. Angalia chujio lao. Unaweza kuona kile wanachopenda. Angalia yale waliyo nayo. Upendo, wanapenda nini? Bi Laodikia ambaye anaelekea kwenye Hukumu ya Mungu. Hiyo ni kweli. Upendo, upendo wa kanisa leo ni kwa ajili ya Laodikia, dhehebu kuu, shirika kubwa, kuu, kitu mashuhuri, watu waliovalia vizuri, wenye tabia nzuri sana, waliojaa hekima, waliojawa na ibilisi, chini ya udanganyifu wa kanisa la Kristo . Kuna neno moja tu linalopaswa kuwa mle ndani, "mpinga Kristo." Kwa kuwa, kila kitu alichofundisha Kristo, wao wanapinga karibia kila kitu; kweli, kutosha tu ili waweze kujiita wenyewe hivyo.

Sasa kama ninyi ni watu wenye busara usiku wa leo, hapa na huko katika nchi ambako Ujumbe unaenda, shauku yenu itakuwa ladha ya Biblia, si ladha ya kimadhehebu, kwa kuwa mtahukumiwa kwa Biblia yenyewe, Neno ambalo ninawaomba mchuje nafsi zenu. Na kukataa Neno moja Lake, na usiiruhusu nafsi yako ipitie kwenye hilo Neno moja, utakataliwa. "Kwa maana mtu hataishi, apumue, kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

Nalo litaletwa kwako, limechaguliwa tangu awali. Na wakati Bwana anapokupulizia, Roho Wake atalihuisha Neno hilo kwa kweli, nawe utaona ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Loo, jamani!

79 Achana na madhehebu ya ulimwengu, pakti ya kidini. Hebu liwekwe kama ile pakiti ya sigara mwituni. Hebu ioze na kuharibika. Ni—ni chujio baya. Na uchukue Neno, ambalo ni Kristo, linalotoa, na kufikia, na kuhifadhi ladha ya Uzima wa Milele, kwa kila mtu atakayelichukua, Uzima wa Milele.

Neno, kama umechaguliwa tangu awali, mnaliona. Hakuna njia ya kulificha toka kwako. Unaangalia pale na kusema, "Mbona, ni dhahiri sana mbele za uso wangu! Ningeliangalia; Hilo hapo. Ninaliangalia moja kwa moja. Ninaliona. Hili hapa, Neno; kila Neno, Neno tu kwa Neno, likiishi." Kisha kuna ladha ya Uzima wa Milele unayotaka.

Na wakati unapovuta pumzi kupitia katika Hilo, ni kitu gani kinachoweza kupitia katika Hilo, Chujio la Mungu? Hakuna kitu ila Roho; hakuna ulimwengu, hata kidogo; hakuna kutokuamini, hata kidogo. Ni Chujio la Mungu. Na unapovuta pumzi kupitia katika Hilo, hakuna kitu kinachoweza kupitia Kwake ila Roho Mtakatifu.

80 Sasa una ushahidi wa Roho Mtakatifu, unaona, ladha ya mwanamume mtakatifu au ya mwanamke. Wao wanataka kuishi. Wana Uzima wa Milele. Na kwa sababu Neno hili limehuishwa kwao, wanaishi; Chujio la mtu mwenye busara, na ladha ya mtu mtakatifu.

Usiuchukue ulimwengu, kama hizo kampuni za sigara, chini ya udanganyifu, bali chukua Chujio halisi la mtu mwenye busara. Chuja pumzi unayopumua, chakula unachokula, kila kitu ulicho; ipumue kupitia katika Neno la Mungu, nawe utakuwa na ladha ya mtu mtakatifu. Kwa kuwa, kitatoa hiyo, kwa kuwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

Nami ninajua, kama tuko au kama hatuko … Ninaamini ndivyo tulivyo. Lakini, kama sivyo tulivyo, kuna mtu ulimwenguni leo ambaye ni sehemu ya Mwili wa Kristo; na Huo utaishi tu kwa Neno la Mungu, kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu kwa ajili ya wakati huu tunaoishi sasa.

81 Nami siwezi kuona ambapo dhehebu … Maneno hayo dhahiri sana katika Biblia, yalisema yangetukia, na mambo ambayo yangekuwako, na hapa tukiishi moja kwa moja katikati yake sasa. Siwezi kuona mahali ambapo ingeweza kuwa kitu kingine chochote ila hiki.

Kanisa, ninatambua sina budi kusimama pamoja nanyi katika Hukumu siku moja. Na iwe mbali nami kuwaambia jambo lo lote la makosa, kwa ajili ya kupendwa na watu. Sitaki jambo hilo. Kama ningekuwa na shauku yangu, ningekuwa, shauku yangu tu ya kibinadamu, ningechukua bunduki yangu na kwenda mwituni na kujijengea kibanda, na kutega, maishani mwangu mwote. Ninazeeka, nimechoka, nimechakaa, na nimeisha moyo, lakini siwezi kuacha. Kuna kitu fulani ndani yangu, kinasaga. Ole wangu kama sisemi Kweli na Kweli yote. Ole wangu nisiposimama hapa mpaka pumzi ya mwisho ya mwili itakaponiacha. Sina budi kusimama, haidhuru mtu mwingine yeyote anasema nini. Ninawajibika mbele za Mungu.

82 Nami kweli ninaamini ya kwamba mambo tunayohubiri ni Kweli. Si kwa sababu ni mimi ninayeihubiri. La, ndugu yangu. La, bwana. Mungu anaujua moyo wangu. Jinsi ningependa kuketi katika kusanyiko na kuwasikiliza wapakwa mafuta wakihubiri. Ingekuwa rahisi jinsi gani kwangu, hakika kwa sababu ningekuwa na Uzima wa Milele kama yule mtu mimbarani. Mimi ni sehemu Yake kama vile alivyo. Ningeenda Mbingu ile ile, niwe na majaliwa yale yale. Ingekuwa ni rahisi jinsi gani kwangu mimi kukaa kule na nisipate michubuko hii yote, na kupigwa, na kufanyiwa yasiyofaa. Ingekuwa rahisi iliyoje, kwa kuwa huko nje usiku kucha bila kulala, saa moja na nusu, ama saa mbili; kushindana usiku kucha na mambo yaliyojitokeza. Ni rahisi jinsi gani kwangu kufanya hivyo, kuchukua bunduki yangu kesho yake asubuhi, fimbo yangu ya kuvulia samaki, na kwenda kuvua samaki ama kuwinda! Jinsi ingekuwa rahisi! Ndugu, kura imeniangukia. Mungu na anisaidie nisijiepushe kamwe na wajibu wangu wa kazi, bali kusimama mwaminifu na wa kweli, na kuwaletea Chujio la mtu mwenye busara litakalokupa ladha ya mtu mtakatifu.

Chujio la mtu mwenye busara ni maji, maji ya farakano. Ni utakaso wa dhambi, ambao ni Neno la Mungu. Na mtu mwenye busara, mtu anayejua hana budi kusimama mbele za Mungu, anajua hana budi kuwajibika kwa kila Neno la Biblia, litaridhisha ladha hiyo iliyo moyoni mwako. Mungu na atusaidie kulipokea, tunapoinamisha vichwa vyetu.

83 Mungu mpenzi, saa nyingine moja ama mbili zimepita. Saa imezunguka sasa. Ujumbe sasa unaingia katika historia, na umeandikwa kwenye kile Kitabu. Sisi sote hatuna budi kujibu sasa kwa ajili ya jambo hili, kila hatua tuliyofanya, kila neno tulilosema, kila wazo lililopitia niani mwetu, rekodi ingali inacheza. Nao utaendelea mpaka uhai utakapokwisha, na ndipo tutajibu kwenye Siku ya Hukumu.

Ee Mungu, Muumba mkuu wa mbingu na nchi, ambaye tunamwamini, ninawaombea watu hawa wa siku hizi. Ninajiombea pamoja nao, ya kwamba Bwana Yesu, ya kwamba utashikilia Chujio Lako. Na kama ninasema jambo lo lote la kukufuru, Bwana, mimi … moyoni mwangu sijui. Ninaomba ya kwamba kama ni kosa kwangu kuchukua Neno Lako na kutumia kitu kama hicho, Wewe nisamehe kwa hilo.

84 Lakini, Bwana, nilifikiri wakati ulipozungumza nami kule msituni, unajua wakati wa asubuhi, nisingeweza tu kuliondoa mawazoni mwangu. Nilikubali kama linatoka Kwako. Kwa hiyo, Baba Mungu, tayari nimesema jambo hilo. Nami ninaomba, Mungu, ya kwamba utaliacha liwe namna nilivyowazia kuwa, ya kwamba mtu mwenye busara, mtu huyo kama ana mawazo yo yote, atajua hana budi kusimama Mbele ya Mungu, naye hataingiza ndani ya nafsi yake cho chote kinachochafua au kilicho kinyume cha Neno la Mungu.

Na, Baba, tunatambua ya kwamba, kama nilivyolilinganisha na madhehebu haya ya siku hizi; si kuwa tofauti, Bwana. Utanihukumu, siku moja, kutoka moyoni mwangu. Nami ninaomba, Mungu, ya kwamba utaona ya kwamba haikuwa kusudi nitofautiane nayo, bali ilikuwa ni kuwa mwaminifu, kujaribu kuwa mwaminifu, nikitambua kwamba ninashikilia ununuzi wa Damu Yako, kutoka pwani hata pwani, sasa hivi,

mkononi mwangu. Na wengi wao wameiamini Ripoti hiyo.

Na, Mungu wa Mbinguni, jalia kusiwepo na mmoja wao atakayepotea. Ninawadai, kila mmoja, na kushikilia mbele yao Chujio la dhambi, Maji ya farakano, Damu ya Yesu Kristo, Neno lililofanyika mwili. Tujalie, Bwana. Na jalia Roho Mtakatifu amimine kupitia kila ahadi, katika nafsi zetu. Na jalia tuwe wawakilishi walio hai wa Bibi -arusi wa Yesu Kristo, katika wakati wa macho, wa kuona katika Nuru ya jioni, kwa kuwa tunawakabidhi Kwako katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

85 Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Mnaamini jambo Hilo? ["Amina."] Mimi, kama nilisema jambo lo lote baya, kwa kusema, "chujio la mtu mwenye busara," siwezi kusema zaidi. Sina elimu. Inanibidi tu kusema kile kinachonijia. Na nilipoona jambo hilo limewekwa pale, nikawaza, "Ni unafiki wa namna gani!"

Ndipo kitu Fulani kikasema, "Kama tu vile kanisa."

Chujio la mtu mwenye busara! Loo, jamani! Kuna zaidi ya hayo. Mtu mwenye busara asingeitumia kamwe. Mnaona? Bila shaka sivyo. Na inatamani ladha ya mtu anayevuta sigara, hiyo ni kweli, kwa sababu hana budi kuwa nayo kuridhisha ladha yake. Lakini mtu halisi, mwenye busara anayejua nafsi yake inaenda Hukumuni, atachuja ladha yake kupitia Neno la Mungu. "Kwa maana wote alionipa Baba watakuja Kwangu." Naye ataishi kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu, ambalo ni Maji ya farakano yanayotutenga na dhambi. Kwa kuwa, inapokuja kupitia kwa Neno, tunaona ya kwamba ni dhambi kutokuamini, kwa hiyo tunaliamini tu na kuendelea. Ni kujitenga na dhambi. Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.]

Nampenda, nampenda …

Hebu na tuinue tu mikono yetu sasa Kwake.

Kwa sababu Yeye alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Kwenye mti wa Kalvari.

86 Yeye alisema nini? "Hivyo watu wote watajua ya kwamba ninyi ni wanafunzi Wangu, mkipenda, iweni na upendo mmoja kwa mwingine." Sasa hebu na tupeane mikono na mtu fulani tunapoimba tena, na kusema, "Ninakupenda, pia, ndugu."

Nampenda, na … (Hii ni kuwajulisha ya kwamba …)
… Yeye alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Kwenye mti wa Kalvari.

87 Sasa, mnapenda Chujio la mtu mwenye busara? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Unapoenda mtaani kusugua mikono na ulimwengu kesho, ndugu, dada, una Chujio la mtu mwenye busara? Wakati mtu huyo anapokuita mtakatifu anayejifingirisha, je! Unatumia Chujio la mtu mwenye busara? Wakati mtu huyo anaposema jambo baya juu yako, je! Una Chujio la mtu mwenye busara? Unaona, tenda mema kwa maovu. Waombee wale wanaokutumia vibaya, na wale wanaokutesa, basi unapumua kupitia Chujio la mtu mwenye busara.

88 Kwa maana kama mkiwapenda wale tu wanaowapenda ninyi, kama tulivyopeana mikono sisi kwa sisi, kama wapendwa sana katika Bwana, hilo ni zuri, lakini je! Mnaweza pia kuwapenda wasiopendwa? Hilo ndilo Chujio la mtu mwenye busara. Huyo ni Roho wa Kristo ndani yako, akiwapenda wale wasiokupenda, ndipo una thawabu ya Mungu. Lakini, sasa, kama ukifanya hivyo kama wajibu, bado huna yule mtu mwenye busara … Uko tu kwenye mzunguko wa pili. Lakini ni kutoka moyoni mwako unampenda kweli, basi unapumua kupitia Chujio la mtu mwenye busara. Na inaridhisha ladha ya mtu mtakatifu, ambayo unajua, kutoka moyoni mwako unamsamehe kila mtu, kila kitu, haidhuru ni jambo gani lililotukia. Yeye si ni wa ajabu?

… Kwanza alinipenda
Na kununua wokovu wangu
Kwenye mti wa Kalvari.
Tutatembea Nuruni, ni Nuru nzuri,
Inakuja ambapo matone ya umande wa rehema ni angavu;
Angaza kote kutuzunguka mchana na usiku,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.
Tutatembea katika Nuru hii, ni Nuru nzuri sana;
Na inakuja ambapo matone ya rehema yaliyochujwa yanaangaza;
Loo, tuangazie mchana na usiku,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.
Njoni, enyi watakatifu wote wa Nuru, tangazeni,
Yesu, Nuru ya ulimwengu;
Ndipo kengele za Mbinguni zitalia,

Yesu, Nuru ya ulimwengu.
Loo, tutatembea Nuruni, ni Nuru nzuri sana;
Inakuja ambapo matone ya umande wa rehema ni angavu;
Loo, tuangazie mchana na usiku,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Mnapenda jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.]
Loo, tutatembea katika Nuru hii, ni Nuru nzuri sana;
Na inakuja ambapo matone ya umande wa rehema ni angavu;
Angaza kutuzunguka mchana na usiku,
Ni Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Ninaupenda tu huo!
Imani yangu inakuangalia Wewe,
Ewe Mwana -Kondoo wa Kalvari,
Ee Mwokozi wa Kiungu;
Nisikie sasa ninapoomba,
Chukua dhambi zangu zote … (Nichuje, Bwana, kupitia Neno.)
Ee, hebu niache tangu leo
Kuwa Wako kabisa!

Hebu wazia tu jambo hilo, likachujwa kupitia Neno, "Wako kabisa."
Wakati ninapotembea gizani maishani,
Na huzuni ikanizunguka,
Uwe Wewe Kiongozi wangu;
Agiza giza ligeuke kuwa mchana,
Futa hofu ya huzuni,
Wala usiniache nipotee
Kutoka Kwako kando.

[Ndugu Branham anaanza kuvumisha Imani Yangu Inakuangalia — Mh.]
… Kwa moyo wangu unaozimia,
Bidii yangu huvuvia;
Amuru giza ligeuke kuwa mchana,
Na kuyafuta machozi ya huzuni,
Ee, hebu niache tangu leo
Kuwa Wako kabisa!

89 Mungu mpenzi, tunapenda kukuimbia Wewe, kwa kuwa hapo ndipo tunapoonyesha hisia zetu, mhemko wetu, kusanyiko lote, unapotupulizia Neno la Uzima. Tunashukuru sana, Bwana. Na wimbo huo, utupokee, sivyo, Bwana? Hiyo ndiyo shauku yetu, ni kuchujwa kupitia Neno la Mungu, kutembea kila siku katika Nuru, Nuru ya Injili.
Na jaze njia yetu kila siku kwa upendo,
Tunapotembea pamoja na Hua wa Mbinguni;
Hebu na twende wakati wote, kwa wimbo na tabasamu,
Jaza njia yetu kila siku kwa upendo.

Tujalie hilo, Bwana. Tubariki pamoja sasa. Jalia neema Yako na rehema ziwe pamoja nasi. Waponye wagonjwa na wanaoteseka kote nchini.

Tunakushukuru kwa ajili ya Ndugu Coggins usiku wa leo, ya kwamba ulimwacha aondoke hospitalini, aende nyumbani akiwa mzima. Asante kwa mambo yote ambayo umefanya, na kwa ajili ya nguvu zetu wenyewe tunajisikia tumeinuliwa sasa.

90 Tunakushukuru kwa ajili ya Ujumbe mdogo uliokatwa katwa usiku wa leo, Bwana. Si—sikuufanya vizuri, bali ninaomba, Bwana, ya kwamba utaufanya vizuri mbele za watu, wapate kuona na kujua ulichokusudiwa. Jipatie utukufu kutoka kwake, Bwana, na jalia tuwe na ufahamu huu, kama hakuna kitu kingine, kwamba yatupasa kuishi kwa Mkate wa Neno la Mungu, uliochujwa kutoka kwa Mungu kwa ajili ya watoto Wake tu. Ni kusanyiko lililotengwa. Si kwa ajili ya mtu mwingine yeyote. Ni kwa ajili ya hao tu, wateule Wako, kama vile yale maji ya utengano ya damu ya yule ng'ombe mke mwekundu yalivyokuwa kwa ajili ya kusanyiko la Israeli tu. Kwa hiyo, Baba, tunajua ya kwamba Mkate huo ni kwa ajili ya Kondoo pekee.

"Si vema mimi kuchukua chakula cha watoto na kuwatupia mbwa," kasema Yesu.

Na mwanamke yule, kwa kujibu, akasema, "Naam, Bwana, hiyo ni kweli, lakini niko tayari kuokota makombo."

Nasi tunajisikia hivyo usiku wa leo, Bwana. Tunataka yale yote unayoweza kutupa, Baba, kwa kuwa tunaona njaa na kiu zaidi kwa ajili Yako.

Tujalie kwamba njaa zetu zitashibishwa na shauku zetu zitajulikana, kwa kuwa, Baba, tunataka kuwa na shauku ya mtu mwenye haki. Na yule Mtu mwenye haki alikuwa ni Yesu Kristo, na shauku Yake ilikuwa ni kufanya mapenzi ya Baba, ambayo alikuwa ni Neno. Tujalie hilo, Baba. Tunaomba katika Jina Lake. Amina.

Hebu na tusimame sasa tunapoimba wimbo wetu wa kufumukana, wa, Peleka Jina La Yesu.

91 Huko nje kila mahali sasa, ambapo Ujumbe umekwenda usiku wa leo, Mungu na awe pamoja nanyi tunapoondoka kwenye maombi. Hebu kila mmoja wenu, huko nje, natumaini mmefurahia kusikiliza kama vile nilivyofurahia kuwaleteeni huo. Nami ninatumaini ya kwamba Mungu ataliweka mioyoni mwenu na kuwapa tafsiri yake sahihi.

Na ninyi watu hapa katika kusanyiko ambao mna leso hizi zimewekwa hapa, nimeziwekea mikono. Ninaomba ya kwamba Mungu atamponya kila mmoja wenu, hakutakuwako na wagonjwa wowote miongoni mwetu, mnaona jinsi Mungu wetu anavyojibu maombi.

Tunapokusanyika pamoja, "Watu walioitwa kwa Jina Langu watakusanyika pamoja na kuomba, ndipo nitasikia kutoka Mbinguni." Yeye aliahidi kufanya hivyo.

92 Kwa hiyo, hatugawanyiki. Sisi ni Mtu mmoja tu; sisi sote ni mmoja, katika Kristo Yesu. Na kila mmoja akimwombea kila mmoja; ninyi niombeeni ninapowaombea. Na Mungu akubariki mpaka tutakapowaona tena.

Nami ninatumaini ya kwamba mtakuwa daima … ninyi mnaoishi hapa karibu, mtakuja kwenye maskani na kumtembelea mchungaji wetu mzuri, Ndugu Neville. Atakufanyia mema, Ndugu Mann na watu wazuri walio nao hapa maskanini.

Kama uko karibu na Ndugu Junior Jackson ama baadhi ya hao wengine kote nchini, New York na mahali mbalimbali ambapo wana mikutano yao, kote kote Arizona na California, tembelea makanisa hayo kama uko huko nje. Tunaomba ya kwamba utarudi tena na kumruhusu mchungaji akusaidie kujua zaidi kuhusu Bwana Yesu.

93 Mungu akubariki sasa tunapoimba Peleka Jina La Yesu.

… Jina la Yesu pamoja nawe,
Mwana wa huzuni na wa maskitiko;
Litakupa furaha na faraja,

[Ndugu Branham anazungumza na mtu fulani jukwaani — Mh.]

… uendako.
Thamani (thamani), Na tamu! (Na tamu!)
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Thamani, Na tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

94 Nikiangalia kusanyiko usiku wa leo, nikimwona Ndugu Estle Beeler kule nyuma, Ndugu Palmer, na wengi, Ndugu J. T., na wahudumu wengi wanaosimama hapa, siwezi kuita majina yao yote. Laiti ningeweza kuwa pamoja nanyi, kila mmoja, hapa juu, na ninyi nyote mliruhusu kusanyiko kuondoka ama mfanye jambo fulani. Mnaelewa, sivyo? Ninajua mna moyo wa Kikristo na mnajua ya kwamba hatuna budi … jinsi tu—jinsi tulivyo; sisi kwa jumla ni Mtu mmoja, katika Kristo Yesu.

Sasa hebu na tukumbuke aya hii inayofuata tunapoimba, wakati Ndugu yetu Martin hapa atatutawanya kwa maombi. Nami nataka kuninii … Huyu ni Ndugu Earl Martin kutoka, ninaamini, kutoka Arkansas ama—ama Missouri. [Ndugu Earl Martin anasema, "Missouri." - Mh.] Missouri, moja kwa moja kule Arkansas, kwenye mpaka wa Missouri pale. Wana kanisa kule.

Nami nikamwona huyu ndugu mwingine kutoka kule chini, siwezi kukumbuka jina lake, Brewer. Alikuwa hapa asubuhi ya leo. Nabashiri angali yupo hapa usiku wa leo. Naam, ninamwona amesimama juu hapa, Ndugu Brewer. Niliahidi kupitia na kuyaweka wakfu makanisa yao, mara nyingi sana. Nitafika huko siku moja, kwa msaada wa Bwana, niwezavyo.

Sasa, tunapoimba aya hii ifuatayo sasa.

Tukiinama mbele ya Jina la Yesu,
Tukisujudu miguuni Pake,
Mfalme wa wafalme Mbinguni tutamvalisha taji,
Wakati safari yetu ikishakamilika.

Hebu na tuuimbe sasa.

Tukiinama mbele ya Jina la Yesu,
Tukisujudu miguuni Pake,
Mfalme wa wafalme Mbinguni tutamvalisha taji,
Wakati safari yetu ikishakamilika.
Jina la thamanii (Jina la thamani), Lo ni tamu iliyoje! Lo ni tamu iliyoje!)
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Lo ni tamu iliyoje!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.
Loo, Peleka Jina la Yesu uendako.
Akiwa ngao kutoka kila mtego; (sikilizeni sasa)
Loo, Wakati majaribu yanapokukusanyikia, (unapaswa kufanya nini?)
Upumue tu lile Jina katika maombi.
Jina la thamani, Lo ni tamu iliyoje!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Lo ni tamu iliyoje!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu.

Jina la thamani, Lo ni tamu iliyoje!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Jina la thamani (kubatizwa ndani Yake; kuomba ndani Yake), Lo ni tamu iliyoje!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

Ndugu Martin. [Ndugu Martin anaomba — Mh.]

MESSAGE hub online
www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7